SportPesa
JACKPOT BABA LAO!
TZS. 288,541,640
CHEZA SASA KWA 1000/= TU!
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Jaji** Mkuu awaonya mahakimu mitandao ya kijamii, marafiki

UKURASA 3



Nipashe JUMAPILI
Jumapili Julai 17, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0581009 ★
www.ippmedia.com
...itter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# WHO, CDC zajitosa uchunguzi ugonjwa ulioibuka nchini

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2
**WACHUNGAJI WAPEWA MIEZI MITATU KUREJEA**
ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Evangelistic Assemblies Of God Tanzania (EAGT), Dk. Brown...

UKURASA WA 4
**MWINYI AVIKINGIA KIFUA VIKOSI SERIKALI UJENZI**
RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametetea uamuzi wa Serikali ya Mapinduzi

UKURASA WA 4
**AWESO AWATUMIA SALAMU WAHUJUMU MIRADI YA MAJI**
WAZIRI wa Maji, Juma Aweso, amesema wizara yake haitawachekea watu ambao...



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Shekhe Rashid Hamad Othman ambaye ni mlezi wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud, wakati alimpomtembelea nyumbani kwake, Utaani, Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba jana. **PICHA: IKULU**

## Waziri Gwajima aliangukia kanisa ukatili wa kijinsia

UKURASA 3

## Majaliwa avunja ukimya fedha michango ya elimu

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA YASHUSHA MAJEMBE MAPYA UK.24
**MAONI, KATUNI** UK.6

# WHO, CDC zajitosa ugonjwa usiojulikana

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imekubali ombi kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) na Kituo cha Kukinga na Kudhibiti Magonjwa (CDC) kutoka Marekani kuongeza nguvu kwenye timu ya wataalam walioko mkoani Lindi ambao kwa pamoja wanafuatilia ugonjwa usiojulikana.

Jumanne ya wiki hii, Rais Samia Suluhu Hassan, wakati akihutubia Mkutano wa 20 wa Shirikisho la Baraza la Maaskofu Katoliki Afrika Mashariki na Kati (AMECEA), alitangaza kuwapo kwa ugonjwa huo Lindi na siku iliyofuata Wizara ya Afya ilitangaza vifo vya watu watatu.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliyasema hayo jana mkoani Kilimanjaro kuwa tayari timu ya wataalamu wa ndani kwa kushirikiana na wa WHO wako Lindi wakiendelea na utafiti wa ugonjwa huo.

Ummy alitoa kauli hiyo jana wakati Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akifungua jengo la nyota tatu la Maabara ya Taifa katika Hospitali Maalum ya Magonjwa Ambukizi Kibongoto wilayani Siha.

"Mheshimiwa Makamu wa Rais, serikali imeshatoa msimamo wake wa kutokuficha maradhi yanayoibuka nchini ndiyo maana tumeruhusu WHO pamoja na wataalamu wengine wa Marekani kwa kushirikiana na wa kwetu kufanya uchunguzi na sasa wako mkoani Lindi," alisema.

Juzi, Waziri Ummy alipokuwa akizungumza kwenye Kikao cha 22 cha Kisekta cha Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kilichofanyika jijini Arusha, alisema serikali imeridhia ombi hilo la WHO na CDC.

Alisema sampuli za vipimo vya maabara zilizochukuliwa kutoka kwa wagonjwa zimeonyesha siyo ugonjwa wa Ebola, Maburg wala UVIKO-19.

Jumatano ya wiki hii, Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, akitoa taarifa za ugonjwa huo, alisema wagonjwa 13 wanaoishi katika kijiji cha Mbekenyera, wilayani Ruangwa mkoani humo, wamegundulika kuwa nao na watatu kati yao wamefariki dunia.

Dk. Sichalwe alisema Julai 7, mwaka huu, Wizara ya Afya ilipokea taarifa kutoka kwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Lindi ikitaja kuwa katika wilaya ya Ruangwa kumekuwapo na ugonjwa usiofahamika kutoka kituo cha Afya Mbekenyera.

Alisema taarifa hiyo ilisema ndani ya siku tatu kuanzia Julai 5, mwaka huu, walipokea wagonjwa wawili katika kituo hicho wakiwa na dalili za homa, kutokwa damu (hususani puani) kichwa kuuma na mwili kuchoka.

**UZINDUZI MAABARA**

Dk. Mpango akizindua maabara hiyo jana Hospitali ya Kibongoto aliitaka Wizara ya Afya kuongeza kasi katika kutafiti na kubaini aina ya mlipuko wa magonjwa kabla haujaathiri jamii.

Pia aliitaka wizara ianzishe ushirikiano endelevu na taasisi za utafiti za duniani kuhusu magonjwa ili kubadilishana utaalamu na ujuzi kulingana na magonjwa yanavyobainika.

Dk. Mpango alisema ushirikikiano huo utalisaidia taifa katika kukabiliana na magonjwa mbalimbali yanapojitokeza.

Alisema kulingana na mabadiliko ya teknolojia serikali imekusudia kuwekeza katika sayansi na ubunifu ili kukabiliana na vita vya maradhi ambavyo ni tishio duniani.

Awali, Ummy alimweleza Dk. Mpango kuwa maabara hiyo haitajikita katika ugonjwa wa Kifua Kikuu pekee bali pia na magonjwa mengine ya kuambukiza ambayo ni hatari.

Alisema uzinduzi huo unafanya kuwepo kwa maabara jamii mbili ambapo moja ipo Dar es Salaam.

Akisoma taarifa ya mradi huo unaogharimu zaidi ya Sh. bilioni 12, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi alisema ujenzi huo umefikia asilimia 99 ingawa wamemuongezea mkandarasi muda ili aweze kuwasaidia wataalamu katika utumiaji wa mitambo.

Alisema mradi huo umejengwa kwa awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza ilijengwa sakafu iliyogharimu zaidi ya Sh. bilioni tisa na ya pili ikihusisha ufungaji mitambo iliyogharimu zaidi ya bilioni 6.23.

Alisema maabara hiyo itatoa huduma za uchunguzi wa magonjwa ya Ebola, VVU na Ukimwi, UVIKO-19, Dengue, Chikungunya na Influenza.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kagaigai alisema mkoa huo upo shwari ingawa unakabiliwa na tatizo la ukame.

**■Imeandaliwa na Romana Mallya (DAR), Mary Mosha na Anjela Mhando (SIHA).**



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizindua mnara maalum unaoonyesha kuanza kwa Hospitali Maalum ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto na huduma zinazotolewa, kabla ya kufungua Maabara ya Afya ya Jamii hospitalini hapo, wilayani Siha, mkoani Kilimanjaro jana. Wa (tatu kulia) ni Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu. **PICHA: OWM**

# Majaliwa avunja ukimya michango shule

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amevunja ukimya kuhusu michango huku akiweka bayana kwamba serikali haizuii kuchangia maendeleo ya shule bali inakataza michango ya hovyo hovyo kwa wanafunzi isiyo na tija.

Akizungumza jana na wananchi wa kata ya Mtoa wilayani Iramba baada ya kuweka jiwe la msingi ujenzi wa Kituo cha Afya Mtoa katika mwendelezo wa ziara yake mkoani Singida, Majaliwa alisema serikali inaruhusu michango inayokubalika.

"Hatuzuii kuchangia maendeleo ya shule tunachokataza ni ile michango kwa mfano mwalimu anamwagiza mwanafunzi alete Sh. 500 ambayo haijapitishwa na kamati za shule au na wazazi," alisema. Majaliwa alisema serikali imeondoa ada kwa wanafunzi kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha sita ili kuruhusu wanafunzi wengi kupata fursa ya kupata elimu.

"Nawaagiza wazazi pelekeni watoto shule sasa hakuna kisingizio cha kukosa ada, michango inaweza ikawapo kwa ajili ya 'kusapoti' maendeleo ya eneo husika lakini kwa makubaliano," alisema.

Kuhusu maji, aliziagiza kamati za maji kusimamia na kulinda vyanzo vya maji na mazingira visiharibiwe.

Waziri Mkuu alisema vyanzo vya maji vimekuwa vikiharibiwa kwa baadhi ya wananchi kuingiza mifugo.

Majaliwa alisema serikali inatumia gharama kubwa katika kutekeleza miradi ya maji kwasababu vyanzo vya maji vimekuwa vikiharibiwa kwa kuchungia mifugo.

Alisema katika mwaka huu wa fedha Serikali itatoa Sh. 5.1 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika jimbo la Iramba Magharibi na Sh.550 milioni zimeletwa kwa ajili ya kufanya utafiti wa wapi maji yatapatikana.

Naye Naibu Waziri Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alisema serikali imepanga kununua magari 195 ya kubebea wagonjwa katika mwaka huu wa fedha wa 2022/2023 ambayo yatagawanywa kwenye wilaya ili kukabiliana na changamoto wanayopata wagonjwa.

Kati ya magari hayo, alisema Halmashauri ya Wilaya ya Iramba itapewa magari mawili.

Aidha, katika barabara, alisema katika mwaka wa fedha uliopita Serikali ilitoa Sh.7.3 bilioni kwa ajili hiyo na mwaka huu zimetengwa Sh.5.6 bilioni kwa ajili kujenga kilometa 2.5 za lami mjini Kiomboi.

# Wachungaji wapewa miezi mitatu kurejea

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Evangelistic Assemblies Of God Tanzania (EAGT), Dk. Brown Mwakipesile, ametoa miezi mitatu hadi Oktoba 22, mwaka huu, kwa wachungaji wanaotaka kurejea baada ya mgogoro kumalizika.

Dk. Mwakipesile alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kumalizika kwa mgogoro ndani ya Kanisa la EAGT uliodumu kwa miaka sita.

Alisema Baraza la Waangalizi wa Kanisa hilo, limetoa miezi mitatu hadi Oktoba 22, mwaka huu, kwa mchungaji anayetaka kurejea baada ya mgogoro kumalizika na kubainisha kwamba uamuzi huo umefikiwa na baraza hilo ambalo ndio chombo chenye kauli ya mwisho ya kukata mashauri mbalimbali kuhusiana na wachungaji.

Alisema Baraza hilo lilifanya uamuzi huo kutokana na kikao kilichofanyika Julai 12, mwaka huu.

Mgogoro wa kanisa hilo ulitokana na aliyekuwa Makamu Askofu Mkuu wa Kanisa, John Mahene, kupinga kuondolewa madarakani kwa sababu za kukiuka miongozo ya imani ya kanisa.

Pia alidai kuondolewa kwa sababu za kuhoji ubadhirifu wa fedha na mali za kanisa uliofanywa na viongozi wa kanisa.

Dk. Mwakipesile alisema Juni 30, mwaka huu, Msajili wa Jumuiya alitoa barua yenye maelezo ya kina ya jinsi serikali ilivyofanya uchunguzi wa kutosha na kubaini kuwa tuhuma zote walizotuhumiwa viongozi wakuu wa EAGT hazina msingi na viongozi hao wakuu hawahusiki na tuhuma zote walizotuhumiwa nazo.

Alisema kutokana na uchunguzi huo, serikali ilitangaza kwamba mgogoro umekwisha na kuwatambua viongozi halali wa Kanisa la EAGT ambao ni Askofu Mkuu Dk. Mwakipesile, Makamu Askofu Mkuu, Dk. Joshua Wawa, Katibu Mkuu Dk. Leonard Mwizarubi, Mhazini Mkuu, Dk. Praygod Mgonja na Mshauri Mkuu, Dk. Livingstone Dennes.

" Kikao hicho ambacho kilifanyika kulingana na Toleo la 2011 Ibara ya XI- 4 kifungu kidogo (f), kilimshukuru Mungu pamoja na serikali kwa kutenda haki na kisha kutoa uamuzi ikiwamo kutoa fursa kwa wachungaji kurejea.

"Mchungaji yeyote anayetaka kurejea baada ya mgogoro kumalizika, atapokewa na ngazi husika kwa sharti la kuandika barua kwa uongozi kwamba ametambua kosa lake na sasa anaomba msamaha na yuko tayari kutumika chini ya uongozi halali wa Kanisa la EAGT," alisema.

## HABARI KITAIFA



Wananchi wa Kimbesa Mpijimagohe, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam, wakihangaika kutoa vitu vyao, baada ya nyumba zao kubolewa na watu waliojulikana kama mabaunsa, siku ya Jumatano wiki hii, wakielezwa kuwa wamevamia eneo hilo, bila kutaja ni nani aliyewatuma, ambapo zaidi ya nyumba 10 zilibomolewa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Jaji Mkuu awaonya mahakimu mitandao ya kijamii, marafiki

**Na Romana Mallya**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahimu Juma, amewaonya mahakimu wapya kuhusu mitandao ya kijamii na kuwataka kujiepusha na matumizi ya teknolojia hiyo pamoja na marafiki ili kulinda hadhi zao.

Pia amewataka wasome Ibara 113 ya Katiba inayosema: 'Ni marufuku kwa jaji wa mahakama ya rufani, jaji wa mahakama kuu, msajili wa mahakama ngazi yoyote, hakimu ngazi yoyote kujiunga na chama chochote cha siasa isipokuwa atabaki na haki ya kupiga kura.

Prof. Juma aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akiwaapisha mahakimu wapya 20 ambao miongoni mwao wanawake ni wanane, wanaokwenda kufanya kazi katika mahakama za mwanzo.

Jaji Mkuu alisema kanuni za maadili za mahakama ni nyaraka muhimu ambazo zitawasaidia kujua mipaka yao ya kimaadili kati yao na familia zao.

"Wakati mwingine mnalaumiwa maadili yenu yamevunjwa kwa sababu ndugu, jamaa na marafiki wamefanya jambo ambalo limehusishwa kwenu. Kuanzia leo (jana) wakati mkipitia hizi kanuni tafuteni muda na familia zenu, mzipitie kwa pamoja kwa sababu nao wameguswa, kuna mambo wanaweza kufanya ukaonekana wewe ndiyo umefanya," alisema.

Aliwataka wawatambue ndugu zao kwa kuhakikisha wanafuata maadili na wawachague marafiki ambao watabaki nao na wengine watakutana nao miaka 30 baada ya utumishi wa mahakama.

"Makundi ya WhatsApp ni maeneo ambayo yanaweza kuwavunjia maadili mkaanza kujadili mambo ambayo hamtakiwi kuyajadili kimaadili. Maisha yenu ni ya upweke, tahadhari unaongea na nani? Unasema nini?, Unachangia nini kwenye mitandao ya kijamii, wengine pengine tuna majina ya bandia tunashambulia kila mtu, tuwe waangalifu sana," aliwaasa.

"Hata mnapokuwa katika upenzi wa jambo fulani lazima mlinde hadhi zenu kwa sababu mapenzi hayo hayawaondolei nafasi zenu. Unaweza kukuta Fei Toto (mchezaji wa Yanga) anafunga bao hakimu unavua shati na kushangilia," alisisitiza.

Pia aliwakumbusha kuwa kanuni hizo hazizungumzii maadili pekee bali zinazungumzia pia uwezo wao na kuwasisitizia kuwa sifa za uhakimu mtu asipojiendeleza zinaweza kupungua au kupotea na kanuni zinaruhusu kukuondoa kwenye uhakimu.

Alisema kwa sasa vyeti vyao havina sifa tena kwa sababu kila siku watakuwa wakipimwa kupitia uamuzi watakaotoa mahakamani, hivyo akawataka mahakimu hao watakapoanza kazi wazingatie maadili ya utoaji haki bila upendeleo na uwajibikaji.

"Sheria unaweza ukasoma, ukajiongeza lakini kama huna maadili, ukishapoteza maadili kurudisha huwa ni ngumu sana, tunasisitiza kwamba maadili ni kiini cha haki, haki isiyo na maadili ni haki ambayo haijitoshelezi na haiwezi kusimama," alisema.

Alisema wanaweza kuwa na uwezo na werevu mkubwa wa sheria lakini wakatumia uwezo wao kupindisha sheria na kuzivuruga ambapo kwenye maadili mahakama imetoa uzito mkubwa.

Jaji Mkuu aliwakumbusha kuwa katiba inawataka kupunguza kupeleka migogoro mahakamani na sheria na kanuni mbalimbali zilizotungwa nazo zinataka waegemee zaidi kwenye usuluhishi ambao hauleti uadui baada ya mgogoro kuisha.

Alisema wakati mwingine wanasheria wamekuwa wakiegemea zaidi kwenye ujuzi wao wa kisheria na kusahau wananchi wanaowafuata kutafuta haki kuwa hawatafuti ufundi walionao.

"Kila shauri linalofika mbele yenu mlipe uzito unaostahili, mkianza kazi katika misingi ya haki miaka 30 ijayo taifa la amani, udugu na umoja litakuwapo lakini mkianza maisha ya utumishi wa mahakama kwa kupendelea, kwa kutotoa haki na kuchelewesha haki, ndoto ya taifa ya udugu haitakuwapo," alisema.

Jaji Kiongozi wa Mahakama ya Tanzania, Mustapha Siyani, aliwataka mahakimu hao wafanye kazi kwa weledi na kujiepusha na vitendo vya rushwa.

"Dhamira yenu ya kwanza iwe ni kutenda haki na si vinginevyo, imarisheni dhana ya mapatano, hamasisheni suluhu katika utatuzi wa migogoro itakayoletwa mbele yenu. Jiepusheni na aina yoyote ya rushwa na ukosefu wa maadili, leo nikiwatazama wote mnang'ara, nina watazama ninawaona mna sura za utukufu.

"Lakini, ninawahakikishieni mkienda kujipaka madoa haitawachukua muda mrefu kabla hamjapoteza nuru ya utukufu wenu, kazi ambayo mmeomba na Mungu amewabariki mmeipata, ni kazi ya kutoa haki," alisema.

Aliwakumbusha mahakimu hao kuwa wamekula kiapo kwa maneno manne na wamesisitiza bila huba, chuki wala upendeleo hivyo siku wakiacha moja ya maneno hayo, ndiyo utakuwa ukomo wa uhakimu wao.

Upatikanaji wao, alisema haukuwa kazi rahisi kwa sababu kwa nafasi zao kulikuwa na maombi takribani 981 na machakato ulihusisha teknolojia ambapo katika hatua mbalimbali za usahili walikuwa wanazungumza na TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano).

Aliwataka watambue kwamba kulikuwa na vijana wengi wenye sifa kama za kwao kutoka maeneo mbalimbali ya nchi.

Jaji Kiongozi aliwakumbusha kuwa wanajiunga na familia ya mahakama katika kipindi ambacho Mahakama ya Tanzania inafanya na inaendelea kufanya maboresho makubwa katika historia ya nchi na moja ya maeneo yanayopewa msisitizo ni matumizi ya TEHAMA katika mfumo mzima wa utoaji haki.

"Mnakwenda kuihudumia jamii ya Watanzania ambayo haiepuki matumizi ya sayansi na teknolojia, ili kurahisisha kazi ya utoaji haki msijiweke mbali na TEHAMA, ufanisi wenu utategemea weledi wenu katika matumizi ya TEHAMA, siyo tu kujua sheria," alisema.

# Waziri aliangukia kanisa ukatili kijinsia

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, ameliomba kanisa kuingilia kati kwa maombi kukomesha matukio ya ukatili kwa wanawake na watoto yanayoendelea kukithiri nchini.

Amesema utafiti mbalimbali uliofanywa na serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) mwaka 2021 unaonyesha kuwa watoto waliofanyiwa matukio ya ukatili nchini ni 11,496 kutoka matukio 15,870 mwaka 2020.

Dk. Gwajima aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akifungua Kongamano la Kitaifa la Wanawake la siku mbili, lililoandaliwa na Mchungaji Rose Shaboka na mume wake, Mtume Nicky Shaboka, kwa ajili ya mafundisho ya neno la Mungu na maombi.

"Huu ndio msaada ninaouomba kwenye kanisa kwa wanaosali na kuomba. Tunahitaji neema ya Mungu kutuvusha hapa. Naomba muungane na wizara yangu kuombea hili tatizo," alisema Dk. Gwajima.

Alisema takwimu hizo zinaonyesha asilimia 60 ya matukio ya ubakaji, ulawiti na kupatiwa ujauzito watoto, wanafanyiwa nyumbani na asilimia 40 shuleni.

Kwa mujibu wa Waziri, wanaofanya matukio hayo nyumbani ni ndugu wa familia ambao wameaminiwa wanaweza kutunza familia wakati wazazi wakiwa kwenye majukumu.

Alisema utafiti unaonyesha kuwa licha ya takwimu hizo, matukio mengi hayaripotiwi na yanamalizwa nyumbani kifamilia.

"Kuna shida kama watu wa Mungu hawatasimama kuomba kwa Mungu kuhusu tabia ambazo zinafanywa na watu wa karibu ambao neno la Mungu limewapita. Wazazi nao hawafuatilii watoto wao kwa sababu wapo bize na majukumu mengine," alisema.

Kadhalika, alisema kwa kipindi cha mwaka jana, matukio ya migogoro ya ndoa yaliyoripotiwa yalikuwa 39,000 na chanzo kikubwa ni kukua kwa uchumi wa wanawake.

"Katika kuinuka kwa wanawake katika nafasi mbalimbali za uongozi, matukio ya ukatili wa kijinsia yanaongezeka," alisema Dk. Gwajima.

Sambamba na hilo, alisema wanawake nchini ni zaidi ya asilimia 51 lakini kati yao zaidi ya asilimia 80 ndio wanaolima na kuzalisha asilimia 60 ya mazao yote ya mazao hivyo wanaume wanaonyanyasa wanawake wanalitakia taifa njaa.

"Wanawake ndio wazalishaji wakubwa wa taifa, wewe mwanaume unayempiga na kumdhalilisha unalitafutia mabaya taifa letu, wapo wanaume wanasema wanafanyiwa ukatili lakini takwimu zao sio kubwa kama za wanawake ambao ndio waathirika wakubwa," alisema Dk. Gwajima.

Aidha, aliwataka wanawake kuchangamkia fursa mbalimbali za mikopo ngazi ya halmashauri, kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi na kumiliki ardhi.

Awali, Askofu Mkuu wa Huduma ya Calvary Assemblies Of God (CAG), Dastan Maboya, alimpongeza Dk. Gwajima kwa kupewa wizara hiyo nyeti ambayo sasa dunia inakabiliwa na wimbi kubwa la matukio ya ubakaji na ukatili mwingine.

"Rais Samia Suluhu Hassan ameamini unaweza kusimamia vyema wizara hii na hivyo wewe unastahili kuisimamia kwa ajili ya utukufu wa Mungu," alisema.

Naye Mchungaji Shaboka alisema lengo la kongamano hilo la wanawake ni kusema na wanawake na kuwajenga kiroho katika kufikia ndoto zao.

# Waziri Mkuu aibua ufisadi wa mil. 350/-

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameibua mianya ya ufujaji mamilioni ya fedha katika wilaya ya Iramba mkoani Singida baada ya watumishi na mawakala kukusanya zaidi ya Sh. milioni 353.6 kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato bila kuzipeleka benki.

Kutokana na hali hiyo, watumishi na mawakala waliofanya ujanja huo, majina yao yamekabidhiwa kwa Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Iramba ili wachukuliwe hatua.

Akizungumza na watumishi wa wilaya ya Iramba katika mwendelezo wa ziara yake kwenye wilaya za mkoa wa Singida, alisema watumishi pekee wanadaiwa Sh. milioni 249 wakati mawakala wanadaiwa Sh. milioni 104 ambazo walizikusanya kwa vipindi tofauti.

Majaliwa alisema miongoni mwa watumishi wanaodaiwa mamilioni hayo ni pamoja na watendaji wa vijiji na kata na baadhi ya wakuu wa idara hali ambayo imesababisha halmashauri kukosa mapato.

Alisema fedha hizo ambazo ni madeni ya muda mrefu, kama zingepatikana zinaweza kujenga zahanati saba kwenye vijiji.

"Sasa tunataka warudishe fedha zetu wala DED (Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri) usimpe kazi hizi RAS (Katibu Tawala Mkoa). Hii ni kazi yako wewe DED," alisema.

Waziri Mkuu alisema inashangaza kuona Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Michael Matomola, amepeleka majina ya watumishi wanaodaiwa fedha hizo Julai 14, mwaka huu, kwa Katibu Tawala Mkoa wa Singida wakati madeni hayo ni ya muda mrefu.

Majaliwa alisema kumekuwa na dosari nyingi kwenye ukusanyaji wa mapato ya ndani na fedha nyingi zinapokusanywa hazipelekwi benki.

Alisema tatizo hili lilishaainishwa hata na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ambaye katika ripoti yake ameeleza kuwa fedha nyingi zinazokusanywa hazipelekwi benki.

"Watumishi hawa madiwani wako chini yenu. Chukueni hatua, mawakala mnawapa kazi ya kukusanya mapato lakini hamuwapi mikataba," alisema.

Aidha, Waziri Mkuu alisema bado kuna udhaifu mkubwa kwenye eneo la usimamizi wa shughuli zinazofanywa na Halmashauri, hivyo lazima wakuu wa idara wawajibike katika kusimamia wenzao na kwamba kila mtumishi ahakikishe anafanya mikutano vijijini kusikiliza kero za wananchi.



Wafanyabiashara wa nyama choma, wakifanya shughuli zao kwenye maeneo ya abiria kusubiria usafiri katika stendi ya daladala Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana, kitendo kinachosababisha usumbufu mkubwa. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Rais Mwinyi avikingia kifua vikosi serikali ujenzi shule

**Na Mwandishi Wetu**

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametetea uamuzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuvipa zabuni ya ujenzi vikosi vya serikali katika ujenzi wa madarasa kwa kuwa vinafanya kazi kwa ufanisi mkubwa.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo mara baada ya kuweka jiwe la msingi mradi wa ujenzi wa madarasa yaliyojengwa kwa fedha za UVIKO-19 Kihinani, Jimbo la Mfenesini, Mkoa wa Mjini Magharibi, ikiwa ni siku yake ya kwanza ya ziara yake anayotarajia kuifanya Unguja na Pemba.

Alisema suala la serikali kutotangaza zabuni za ujenzi huo lilikuwa na maana kubwa kwa kuwa ilitambua viko vikosi vyake ambavyo vina uwezo mkubwa katika ujenzi likiwamo Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU).

Alikipongeza kikosi hicho kwa hatua zake hizo za ujenzi ikiwa ni pamoja na kupunguza fedha za ujenzi wa madarasa hayo tofauti na kampuni ambazo zilitaka kila darasa lijengwe kwa Sh. milioni 50 na badala yake JKU imejenga kwa Sh. milioni 20 kwa kila darasa.

Rais Dk. Mwinyi alisema hatua hiyo ya ujenzi wa madarasa, itapunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya wanafunzi katika madarasa ambapo awali darasa moja lilikuwa likitumika na wanafunzi 200 lakini sasa darasa moja litakuwa na watoto takribani 55.

Pia alisema serikali ina mkakati maalum wa kuongeza kiwango cha elimu na baada ya kukamilika madarasa hatua itakayofuata ni kuongeza idadi ya walimu na kwamba serikali inatarajia kuajiri walimu 4,000, hivi karibuni. Rais Dk. Mwinyi pia alieleza azma ya serikali ya kujenga chuo kipya cha kisasa cha ualimu ili walimu wafundishe kwa ufanisi mzuri zaidi kama ilivyokuwa siku za nyuma.

Dk. Mwinyi alitumia fursa hiyo kwa kuwaahidi vijana wa JKU walioshiriki katika ujenzi huo kwamba mara tu ajira zitakapotangazwa wao ndio watakuwa wa mwanzo kutokana na kazi kubwa waliyoifanya.

Wakati huo huo, Rais Mwinyi aliweka jiwe la msingi katika hospitali mpya ya wilaya, iliyoko Mbuzini, Wilaya ya Magharibi A na kusema kuimarika kwa huduma za afya kunahitaji hospitali za rufani kama zinazojengwa na serikali.

Dk. Mwinyi alisema maendeleo ya nchi yanahitaji kwa kiasi kikubwa huduma za afya pamoja na elimu na ndiyo maana Serikali anayoiongoza imeweka kipaumbele katika sekta hizo.

Pia aliwahakikishia wananchi kwamba Serikali anayoiongoza itahakikisha inafanya kazi ya kuimarisha huduma za jamii.

# Aweso awatumia salamu wahujumu miradi ya maji

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

WAZIRI wa Maji, Juma Aweso, amesema wizara yake haitawachekea watu ambao watajihusisha na kuhujumu miundombinu ya maji ambayo serikali imewekeza kiasi kikubwa cha fedha.

Aweso aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wakazi wa Kata ya Dabalo wilaya ya Chamwino, wakati akiweka jiwe la msingi mradi wa maji uliogharimu Sh. milioni 907.

Alisema, kutokana na azma ya serikali ya kumtua mama ndoo kichwani kwa kuwekeza fedha nyingi katika miradi ya maji, wizara hiyo haitawafumbia macho watu wote ambao wanahujumu miundombinu ya maji nchini.

"Hawa watu ndugu zangu si wa kucheka nao hata kidogo kwani unaweza kucheka na nyenyere(sisimizi) wakati mwingine akakung'ata sehemu mbaya. Kwa hiyo kama mtu amekula akashiba achezee kidevu chake na kitambi chake lakini si miradi ya maji," alisema Aweso.

Pia alisema kutokana na maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan, kwa wizara hiyo kuwaondolea adha ya upatikaji wa huduma ya maji safi na salama wananchi, atahakikisha azma hiyo inafikiwa na kila mtu anapata huduma hiyo bila kikwazo.

"Katika bajeti ya maji iliyokuwa imetengwa, Dabalo haikuwepo lakini kutokana na ombi la mbunge wenu kuhusu kero ya maji mliyokuwa nayo, sisi wizara tumepambana kuhakikisha kiasi hiki cha fedha takribani milioni 907 kinapatikana kwa ajili ya mradi huu," alisema.

Waziri Aweso alipongeza Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa kuendelea kusimamia miradi ya maji katika maeneo ya vijijini na kutoa matumaini kwa wananchi.

"Niwapongeze sana RUWASA kwa namna ambavyo mnatusadia katika kazi zetu kwani wanasema ukiona kobe juu ya mti ujue kapandishwa nyinyi ndiyo mmeifanya kazi yetu kuwa rahisi hongereni sana kwa kutuheshimisha," alisema.

Aweso pia aliipongeza kampuni ya PLASCO iliyojenga tangi la maji katika mradi huo kwa kutumia tekomolini ya kisasa na ya muda mfupi kufunga tangi la maji lenye uwezo wa lita 150,000 kwa muda wa wiki mbili.

Alisema teknolojia hiyo itasadia miradi ya maji kukamilika kwa muda mfupi ikilinganishwa na ile ambayo ilikuwa ikitumika hapo awali.

Mbunge wa Chamwino na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, aliishukuru serikali kwa kuipatia Kata hiyo kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya mradi huo wa maji.

"Mheshimiwa Waziri, kata hii ilikuwa na kero kubwa ya huduma ya maji lakini kwa mradi huu mmetusaidia sana sasa tumebaki na deni la kura kwa Mheshimiwa Rais katika uchaguzi mkuu wa 2025," alisema.

# Maeneo yote kufikiwa na huduma afya

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amesema serikali imedhamiria kufikisha huduma mbalimbali za jamii zikiwamo za afya sehemu mbalimbali vijijini ili wananchi wazipate kwa wakati.

Majaliwa ameyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi katika kata ya Mtoa, wilayani Iramba baada ya kukagua na kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Kituo cha Afya akiwa kwenye ziara yake ya kikazi mkoani Singida.

Alisema kukamilika kwa kituo hicho kutawawezesha wananchi hao kupata huduma za afya zikiwemo za maabara, mama na mtoto na upasuaji karibu na makazi yao.

"Mheshimiwa Rais Samia (Suluhu Hassan) ameelekeza huduma za afya ziwafikie wananchi wote hadi waishio vijijini," alisema.

Waziri Mkuu alisema kwa wilaya ya Iramba, serikali imeidhinisha Sh. bilioni 2.8 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya sita ili kusogeza huduma hizo karibu na wananchi.

Majaliwa pia aliupongeza uongozi wa wilaya ya Iramba kwa usimamizi mzuri wa ujenzi wa kituo cha afya cha Mtoa na kuiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kupeleka Sh. 262, 635,689 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa kituo hicho.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Dk. Festo Dugange alisema wataendelea kusimamia ukamilishaji wa kituo hicho cha afya ili wananchi wa maeneo hayo wapate huduma hizo karibu na maeneo yao ya makazi.

Amesema serikali imeridhia Sh. bilioni 3.1 zitumike katika ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya wilayani Iramba na kati ya hizo, Sh. bilioni 2.8 ni kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya Kisiriri, Mtoa, Urugu, Mwendugemba, Shelui na Tyegele na Sh. milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa zahanati sita katika wilaya hiyo.

Naibu Waziri huyo alisema mbali na fedha hizo, pia serikali imetoa Sh. bilioni 7.4 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara za mijini na vijijini kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) ili kuziwezesha barabara za wilaya hiyo kupitika kwa wakati wote.

Naye Mbunge wa Singida Magharibi ambaye pia ni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alitumia fursa hiyo kumshukuru Rais Samia kwa kuidhinisha fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maendeleo katika wilaya hiyo.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Michael Matomora, alisema kabla ya mradi huo, kata ya Mtoa haikuwa na kituo cha afya, hivyo huduma kwa ngazi ya Kituo cha Afya zilikuwa zikipatikana kata ya Shelui, ambako ni umbali wa kilomita 15.

# Chuo chatoa unafuu Watanzania kusoma nje

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO Kikuu cha Maharishi Markandeshwar cha India, kilichobobea kwenye kozi za afya, kimetangaza kutoa ufadhili wa hadi asilimia 40 kwa wanafunzi watakaopata udahili wa kujiunga na chuo hicho katika mwaka ujao wa masomo.

Chuo hicho kimetoa ofa hiyo huku kikiahidi kushiriki Maonyesho ya Vyuo Vikuu yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), yanatarajiwa kuanza kesho kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam.

Vyuo vingine vya nje vitakavyoshiriki maonyesho hayo yanayofanyika kila mwaka hapa nchini ni kutoka India, Iran Cyprus, Uturuki, Georgia, Canada, Australia, Russia, Marekani na Uingereza.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Elimu Nje ya Nchi, Global Education Link (GEL), Abdulmalik Mollel, ambaye ndiye mwenyeji wa vyuo vya nje vitakavyoshiriki, alisema jana kuwa chuo hicho kina zaidi ya wanafunzi 35,000 ndani ya kampasi moja na hospitali kubwa mbili za wanafunzi kufanyia mafunzo kwa vitendo ndani ya kampasi.

Alisema moja ya hospitali hizo ina zaidi ya vitanda 1,200 kwa ajili ya kuhudumia wananchi wa nchi hiyo na hospitali nyingine kubwa kwa ajili ya kuhudumia wageni kutoka nje ya nchi, hivyo wanafunzi watakaosoma chuo hicho watapata fursa nzuri ya kufanya mafunzo ya vitendo.

Mollel alisema chuo hicho kilichoko katika mji wa Mulana Ambara kilichopata ithibati ya ubora na serikali ya India, kina zaidi ya kozi 350 tofauti kama uhandisi na biashara. "Si tu kusoma, unapaswa kusoma chuo bora chenye viwango vya hali ya juu kama hiki na ndani ya chuo hiki tayari kuna wanafunzi 100 wa Tanzania ambao wamedahiliwa tayari kwa masomo na 200 wameshahitimu na wamerudi wanafanya kazi hapa," alisema. "Sifa nyingine ya chuo hiki ni kwamba kinaanzia shule ya awali mpaka PhD (shahada ya uzamivu) kwa maana kinaanzia shule ya msingi, sekondari, astashahada, shahada, shahada ya uzamili na ya Uzamivu na gharama ni ndogo sawa na vyuo vya ndani," alisema.

Alisema chuo hicho kitatoa ufadhili wa asilimia 40 hadi 50 kwa wanafunzi wa vyuo watakaokwenda kwenye maonyesho ya TCU na kufanikiwa kupata udahili wa papo kwa papo.

Mollel alitaja chuo kingine kitakachoshiriki maonyesho hayo kuwa ni Sharda kilichoko mji wa Great Noida, Delhi India, ambacho ni miongoni mwa vyuo vikubwa India kilichojikita kwenye kozi za afya .

Alisema Great Noida ni mji unaosifika sana nchini India kwa kuwa na vyuo vikuu vingi ambako kuna zaidi ya vyuo vikuu 100 kwenye eneo moja, Sharda kikiwa kimojawapo.

"Kwenye mji wa Great Noida, miongoni mwa vyuo vikuu vitatu bora Sharda kimo ndani, chuo chenye hospitali kubwa yenye zaidi ya vitanda 1,000. Wakati wa mlipuko wa UVIKO- 19, hospitali hii ya Sharda iliteuliwa na serikali kuhudumia jamii ya wagonjwa hao na ni kutokana na maarifa na teknolojia ya hali ya juu," alisema.

"Chuo hiki kina kampasi nne tofauti tofauti ndani na nje ya India na kina wanafunzi Watanzania zaidi ya 100 wanaosoma na zaidi ya 150 ya Watanzania waliohitimu na asilimia 99 ya wanafunzi watanzania wanaosoma hapa wanamaliza kwa alama za juu," alisema

Alisema chuo hicho kina uwezo wa kipekee wa teknolojia ya hali ya juu na ndiyo sababu kampuni kubwa kama Amazon na Microsoft zimekuwa zikiwekeza kwenye chuo hicho na wanafunzi wanaosoma kupata eneo la kufanya mafunzo kwa vitendo.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akifungua bomba la maji wakati akikagua mradi wa maji Misigiri, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, mkoani Singida jana. **PICHA: OWM**

# RC Makalla apongeza hatua za kukabili uhaba wa maji

**Na Frank Monyo**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, ameipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kwa kuchukua hatua kukabiliana na uhaba wa maji msimu wa kiangazi.

Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa ya kutunza maji, hivyo kuwahakikishia wananchi upatikanaji wa huduma hiyo.

Kauli hiyo imetolewa juzi wakati wa ziara za kamati za ulinzi na usalama za mikoa ya Dar es Salaam na Pwani iliyoongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Aboubakar Kunenge, katika mitambo ya Ruvu Juu na Chini kujionea hali ya uzalishaji maji na usambazaji katika mikoa hiyo.

Alisema mwaka jana hali ya upatikanaji maji haikuwa nzuri kutokana na mvua za Oktoba hadi Desemba kutokunyesha na matokeo yake mikoa kukumbwa na uhaba wa maji.

"Mimi na wenzangu tuliokuja hapa tumejiridhisha pasina shaka kuanzia Ruvu Juu mpaka Ruvu Chini tumeona hali ya upatikanaji wa maji iko kwenye hali ya kiridhisha mpaka sasa. Maana yake ni kwamba ziko jitihada zilizofanywa na DAWASA kwani tulivyokuja mwaka jana hali haikuwa hivi. "Wametengeneza bwawa la kuhifadhi maji, jitihada hizi zinapaswa kuungwa mkono na wadau mbalimbali vikiwamo vyombo vya ulinzi na usalama, viongozi na wananchi. Kwa watu wanaochepusha maji na hawana vibali kunaweza kutokea upungufu kwa maana hiyo tunapaswa kudhibiti hali hiyo.," alisema Makalla.

Aliongeza kuwa tuendelee kuwaambia wananchi wanaoishi karibu na vyanzo vya maji watunze mazingira na kuachana na uchepushaji wa maji.

"Hali ya maji iko vizuri lakini tunategemea mvua zitakazoanza Oktoba hadi Desemba zije ziunganishe huu upatikanaji wa maji. Kwa hiyo mvua kama hazitanyesha, hiyo si serikali maana watu hudhani hata mvua zikinyesha ni serikali imesababisha.," alisema.

Katika ziara hiyo, Makalla alijionea kina cha Maji Ruvu Juu kikiwa mita 16 huku Ruvu Chini kikiwa ni mita 4.2 na kubainisha kuwa hali hiyo ni nzuri kwa sasa kwa kuwa kwa mujibu wa DAWASA, kiwango hicho kinaweza kuwavusha salama kipindi cha kiangazi.

Makalla alimshukuru na kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada za dhati anazofanya kuboresha sekta ya maji kupitia miradi mikubwa ya usambazaji maji pembezoni mwa mji. Pia aliipongeza DAWASA kwa kazi kubwa na nzuri inayoifanya kusimamia vizuri miradi ya maji. Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema mamlaka hiyo inaendelea kufanya kila jitihada za kuhakikisha kiasi cha maji kilichopo kinalindwa na kudhibiti upotevu wa maji.

Alisema lengo la ziara hiyo ni kuonyesha jitihada ambazo zimefanyika katika kukabiliana na ukame wa mwezi Septemba hadi Novemba.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua zaidi zichukuliwe kwa wanaohujumu mapato

**KATIKA** siku za karibuni, viongozi wakuu wa nchi wamebainisha kuwapo kwa wizi na ubadhirifu wa fedha za umma katika taasisi mbalimbali za serikali zikiwamo mamlaka za serikali za mitaa.

Wizi huo unabainika kutokana na kuwapo kwa mianya ya ufujaji wa mapato hususan katika miradi mbalimbali ya halmashauri. Miongoni mwa madudu hayo, yameibuka wiki hii katika ziara ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, inayoendelea mkoani Singida.

Majaliwa katika ziara hiyo, alinusa harufu ya ufisadi katika kituo kikuu cha mabasi cha Manyoni unaofanywa na baadhi ya watendaji wa halmashauri na mawakala waliopewa kazi ya kukusanya ushuru wa mabasi katika stendi hiyo. Ufisadi huo ulibainika baada ya serikali kuweka maofisa wake na kukusanya fedha nyingi kuliko zile zilizokuwa zikikusanywa na mawakala, hivyo kubaini kuwa baadhi ya fedha zilikuwa zikiingia mifukoni mwa wajanja.

Kama vile haitoshi, jana katika ziara yake wilayani Iramba, Majaliwa alisema zaidi ya Sh. milioni 350 za mapato ya ndani zimekusanywa bila kupelekwa benki, hivyo kuagiza hatua zichukuliwe dhidi ya waliohusiksa na mchezo huo.

Licha ya hayo kubainika katika ziara hiyo ya kiongozi wa ngazi za juu serikalini, juzi, Taasisi ya WAJIBU chini ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Mstaafu, Ludovick Utouh, iliibuka na hoja ya kuwapo dalili zote za ufisadi wa Sh. Trilioni 1.254 kama zilivyoainishwa katika ripoti ya CAG ya mwaka 2020/21. Ripoti hiyo inaonyesha kwamba fedha hizo 1.254 zilikusanywa na serikali lakini hazikuingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Kutokana na kuwapo kwa taarifa hiyo, taasisi iliishauri serikali kuhakikisha fedha zote inazozikusanya, zipite kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Katiba.

Utouh pia aliishauri serikali kuwawajibisha maofisa wote waliotajwa na CAG kuhusika katika kashfa ya uteketezaji wa noti halali za Sh. bilioni 3.9 kwenye Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ili kuchochea uwajibikaji na utawala bora.

Hiyo ni mifano michache tu juu ya matumizi mabaya ya fedha za serikali kwani kila ripoti ya CAG inapotolewa, kumekuwa kukianikwa madudu mengi katika taasisi za serikali zikiwamo zile zinazotegemewa katika ukusanyaji wa mapato ya serikali ambayo ni muhimu kwa miradi ya maendeleo ikiwamo afya, elimu na miundombinu. Sambamba na madudu hayo, pia kumekuwa kukibainishwa ukiukwaji wa kanuni na taratibu mbalimbali za kifedha zikiwamo za ununuzi wa umma na mikataba ya utekelezaji wa miradi ya serikali.


Moja ya mambo hayo ni mkataba wa uongezaji wa kina katika bandari ya Tanga. Ripoti ya CAG ilibaini mkandarasi aliyepewa kazi ya kuongeza kina cha bandari hiyo na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), alimpa kazi hiyo mkandarasi mwingine bila kutoa taarifa kwa mamlaka.

Kutokana na kubainika kwa madudu hayo, kumekuwa kukitolewa ushauri kwa serikali juu ya nini cha kufanya ikiwamo kuwawajibisha waliohusika na mambo hayo. Serikali inapongezwa kwa kuchukua hatua. Hata hivyo, hatua zaidi zinapaswa kuchukuliwa ikiwamo kuwafikisha wahusika katika vyombo vya sheria.

Tanzania ina rasilimali nyingi na vyanzo vingi vya mapato vinavyotakiwa kusimamiwa ipasavyo ili kukusanya fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo lakini wajanja wachache wamekuwa wakitumia mianya hiyo kujinufaisha huku miradi ya maendeleo ikidorora na lawama kushushiwa serikali.

Ni wakati muafaka sasa, serikali kupitia taasisi zake za kiuchunguzi na zile zinazosimamia uwajibikaji na utawala bora, zikatekeleza majukumu yao ikiwamo kuwachunguza wale wanaojihusisha na ubadhirifu kisha kupelekwa katika vyombo vya sheria. Muda wa Tanzania kufanywa shamba la bibi umekwisha, hivyo wale wanaohujumu rasilimali za taifa wawajibishwe ipasavyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mkakati wa kuacha kupikia kuni uje na matokeo chanya

Na Sabato Kasika

**WAZIRI** wa Nishati, January Makamba, anaendelea na kampeni ya kuhamasisha matumizi ya nishati salama ya kupikia, lengo likiwa ni kunusuru maisha ya Watanzania waishio vijijini, ambako wengi wao wanatumia kuni.

Amechukua hatua hiyo kutokana na kile anachoeleza kuwa Watanzania 22,000 hupoteza maisha kila mwaka kutokana na magonjwa ya upumuaji yanayochangiwa na matumizi ya kuni.

Kwa sasa Waziri huyo yuko mikoani akiendeleza na ziara ya kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala ya kupikia, ikiwa ni utekelezaji wa mkakati huo wa kunusuru Watanzania dhidi ya janga hilo.

Anasisitiza kuwa mkakati huo wa kuhamasisha nishati mbadala ni hatua muhimu kwa kuwa bila kufanya hivyo, matumizi ya kuni yataendelea kugharimu maisha ya Watanzania wengi.

Kwamba, mkakati huo ni wa kisera, kibajeti, kimatumizi, ambapo binafsi ninaamini kuwa mkakati huo ni wa muhimu ingawa umechelewa, kwani matumizi ya kuni au mkaa yamekuwa na madhara tangu muda mrefu.

Waziri huyo anazunguka mikoa 14 na wilaya 38, kwa ajili ya kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala, ili kuhakikisha kwamba jamii inatambua madhara ya kuni na kuachana nazo.

Lakini si kwamba upikaji kwa kutumia kuni kunasababisha tu magonjwa ya upumuaji, bali pia kuna suala la imani za kishirikina ambalo husababisha baadhi ya watu kuuawa.

Ushirikina kivipi? Inaelezwa moshi wa kuni umekuwa ukisababisha watumiaji wa kuni kuwa na macho mekundu, ambapo wekundu huo unatafsiriwa kuwa watu wenye macho ya aina hiyo wachawi na kufikia kuuawa.

Kwa maana hiyo, vifo vinavyotokana na matumizi ya kuni, vina sura mbili, kuanzia magonjwa ya upumuaji, lakini pia macho kuwa mekundu na ambapo wenye imani za kishirikina huwachukulia kama wachawi na kumbe sivyo.

Kwenye suala la nishati mbadala, ninadhani mkakati wa kuachana na kuni ungekwenda sambamba na kuwapo unafuu wa gharama ya nishati hiyo, ili kila Mtanzania aweze kumudu bei yake.

Ikumbukwe kuwa, wengi wanaotumia kuni ni wa vijijini, maisha ya huko yanaeleweka kuwa ni ya hali ya chini, hivyo wakipata nishati mbadala kwa bei nafuu, itawawia rahisi kuachana na matumizi ya kuni.

Lakini pia Waziri huyo wakati akiwa katika Wizara ya Muungano na Mazingira, aliwahi kubainisha kuwa kila mwaka takriban hekari milioni moja ya miti ambayo ni takriban asilimia 70 ya miti inakatwa.

Kwamba miti hiyo hukatwa kwa ajili ya mkaa, ambapo kwa hali hiyo asilimia 61 ya nchi inakabiliwa na jangwa, huku maeneo mengi ambayo mkaa huo unatoka, wakazi wake hawatumii, badala yake unasafirishwa hadi mijini.

Kwa kuwa inaonekana kwamba, matumizi ya kuni au mkaa yanachangia vifo na uharibifu wa mazingira, ni vyema mkakati wa kuacha kupikia nishati hiyo ukawa na matokeo chanya ili kuokoa maisha ya Watanzania.

Ninadhani kwamba, njia mojawapo ni kuhakikisha nishati mbadala inapatikana kwa wingi kote nchini, tena kwa gharama ambayo kila mmoja anaweza kuimudu, hasa gesi ambayo bei yake imeendelea kupaa.

Gesi kwa sasa inaanzia Sh. 20,000, kama itauzwa kwa bei kubwa vijijini, inaweza kuwa vigumu watu kumudu bei yake kutokana na hali halisi ya maisha. Labda mkakati wa Makamba uje na nishati nyingine mbadala wa gesi.

Kuwa na nishati mbadala ni hatua muhimu, kwani bila kufanya hivyo, matumizi ya kuni yataendelea kugharimu maisha ya Watanzania wengi, ila jambo la kuzingatia ni gharama za nishati hiyo kuwa rafiki.

Vijijini unaweza kukuta familia ina watu hata zaidi ya 10. Kwa hali hiyo hata matumizi yao ya nishati yanaweza kuwa makubwa, hivyo kama gharama yake itakuwa ya juu, wanaweza kushindwa kuimudu.

Waziri Makamba endelea na mkakati wa kuwatoa Watanzania hasa wa vijijini, katika hatari ya kupoteza maisha kwa matumizi ya kuni, lakini ingefaa nishati mbadala ipatikane kwa wingi, tena kwa bei nafuu.

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Hatimaye nimeupata uwakili, je, nitakuwa kama Lakha?- 1



Na Pascal Mayalla

**Enzi za Mwalimu Julius Nyerere, Operesheni Vijiji ilipoanza mwaka 1975, ilikuta baba tayari ni bosi kazini kwake na baba yangu mdogo, Mzee Kasanga, ni mfanyabiashara tajiri, hivyo waliisha mjengea mama yao nyumba ya kisasa ya matofali, mabati, kupigwa lipu, rangi na dari wakati nyumba nyingi zilikuwa za udongo na nyasi.**

WAPENZI wasomaji wangu wa safu hii ya "Kwa Maslahi ya Taifa", mimi mwandishi wenu ni miongoni mwa mawakili wapya 335 walioapishwa wiki iliyopita na Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma. Hii ni makala ya shukrani kwa Jaji Mkuu, uongozi wote na wafanyakazi wa mhimili wa Mahakama wakiwamo wa kitengo cha mawakili. Asanteni sana.

Safari yangu ya kutamani kuwa wakili ilianzia Mwanza mwaka 1976, yaani miaka 45 iliyopita nikiwa darasa la pili katika Shule ya Msingi ya Nyakahoja ambapo baba yangu, Mzee Andrew Mayalla, Mungu amlaze mahali pema peponi, alikuwa mtumishi wa serikali tukiishi Isamilo.

Mara ghafla usiku mmoja tumekuja kusombwa mzobe mzobe, sina hili wala lile bila kujua kilichotokea mara tumerudishwa kijijini tena sisi japo ni Wasukuma wa Mwanza, babu mzaa baba 'alikufa akaoza' kwa mwanamke wa Kinyamwezi, akahama Mwanza jumla na kuhamia Tabora. Kwa hiyo alioa Tabora, baba akazaliwa Tabora, akasoma huko na kuoa pia huko.

Kwa hiyo baba aliandika kuwa nyumbani kwao ni Tabora kijiji cha Itonjanda, hivyo ghafla tukarudishwa kijijini!.

Enzi za Mwalimu Julius Nyerere, Operesheni Vijiji ilipoanza mwaka 1975, ilikuta baba tayari ni bosi kazini kwake na baba yangu mdogo, Mzee Kasanga, ni mfanyabiashara tajiri, hivyo waliisha mjengea mama yao nyumba ya kisasa ya matofali, mabati, kupigwa lipu, rangi na dari wakati nyumba nyingi zilikuwa za udongo na nyasi.

Kwa hiyo operesheni hiyo ilipoanza, ilikuta tayari nyumba nzuri ya kisasa kijiji kizima, hivyo kutakiwa kuvunja na kuhamia kijijini upande wa pili wa barabara kwa wale wanaonijua kuwa ni mbishi, mimi siyo kwani kuna watu wabishi nchi hii, walimbishia hadi Nyerere. Wazee waligoma kuvunja nyumba na kijiji kizima kilihamia upande wa pili wa barabara, hivyo nyumba yetu ikabaki pekee yake upande huo.

Hebu fikiria, mtoto unazaliwa, unakuta baba na mama ni mabosi wa serikali, asubuhi ni mwendo wa chai ya maziwa, mkate na siagi kwa mayai ya kukaanga.

Baba anaendesha gari aina ya Volvo, mama Volkswagen ya kibanda wazi Mwanza nzima, mtoto unasoma shule ya mchepuo wa Kiingereza (English Medium) Nyakahoja, mara ghafla mnahamishwa usiku usiku na kutupwa kijijini!.

Hapo ndipo unagundua kuwa hata ile nyumba ya Isamilo si yenu bali ya serikali na magari ni ya serikali!. Hadi fanicha za ndani, makochi, vitanda hadi magodoro vyote ni mali ya serikali, mnahama na masanduku tu ya nguo zenu. Baada ya kufika kijijini nikaandikishwa Shule ya Msingi ya Itonjanda.

Enzi za maisha ya Mwanza, miongoni mwa vitu nilivyorithi kwa baba ni roho nzuri, kupenda starehe na kula vizuri. Soda, kuku na keki vilikuwa vyakula vya kawaida enzi za Mwanza. Sasa soda na kuku ni mpaka siku ya sikukuu au wakija wageni na kijijini sasa hakuna tena starehe! Starehe pekee ilikuwa kusikiliza muziki wa santuri na sisi ndio pekee tulikuwa na muziki wa santuri kijiji kizima tena betri zikiisha unafanya kuzianika juani.

**Baba kuchukuliwa**

Siku moja usiku, baba alifuatwa na watu wa kazini kwake mimi nikidhani amesafiri, enzi hizo tukiishi na mama mdogo. Moja ya sifa ambazo si nzuri niliyorithi kwa Baba, ni kupenda warembo.

Mambo ya Wasukuma na wanawake wengi, yaliishamshinda mama yangu kitambo, akaondoka, hivyo mimi nimelelewa na mama wadogo watatu. Naomba tusiwaite mama wa kambo. Baada ya mzee kuchukuliwa, mama mdogo alirudi kwao, hivyo mimi kubaki na bibi.

Baada ya muda si mrefu, baba yangu mdogo, Mzee Mathew Kasanga, alinifuata kijijini Itonjanda, akanipeleka kwake Dar es Salaam, tena tulikuja kwa ndege ya kukodi. Enzi hizo ndege za kukodi ni za jeshi tu na ndege hiyo ilikuwa ikiendeshwa na Captain Sanden na kuanzia hapo nikasema nikiwa mkubwa, nataka kuwa rubani.

Wakati najiunga na familia ya Kasanga, mimi ndiye nilikuwa mtoto mkubwa. Dada yangu Maria yeye aliishatangulia kuchukuliwa akisoma sekondari ya Jangwani. Kutokana na kulelewa na mama wadogo na siku zote mama wa kambo wana sifa mbaya za kutesa watoto wa wenzao, ili kuepuka kuonekana wanatesa, nikajikuta nimelelewa kwa kudekezwa!. Niliingia nyumbani kwa Mzee Kasanga kama mtoto aliyeharibika lakini niko hivi leo, sifa na pongezi ziende kwa mke wa Mzee Kasanga, mama wa Kiganda, Nora Katusabe Kasanga.

Dar tulikuwa tunaishi nyumba nzuri, maghorofa ya Drive In Flats, nikajiunga Shule ya Msingi Oysterbay na kurejea kwenye maisha bora zaidi ya yale ya Mwanza, maana Mzee Kasanga kwenda Ulaya ni kama kwenda Dodoma. Enzi hizo za ile miezi 18 ya kukaza mikanda, sisi kuanzia sabuni, dawa za meno, nguo, viatu na raba vyote ni kutoka mamtoni (Ulaya).

Kipindi chote hiki, mpaka ninatua kwa Mzee Kasanga, sikuwahi kuelezwa rasmi baba alienda wapi na nini kilimtokea. Je, ni nini kilimtokea Mzee Mayalla na kina uhusiano gani na uwakili wa Pasco Mayalla?.

**Tukutane Jumapili ijayo. Wasaalam.**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# RITA mshikeni mkono binti huyu akutumikieni



Na Joseph Kulangwa

**Mungu mkubwa, Anna akasoma miaka yake miwili na kumaliza, tena nako huku akifaulu kwa daraja la kwanza kidato cha sita, akijua kuwa sasa ni yatima hana kwingine kwa kushika, ila ni yeye na Mungu wake. Hongera sana Anna.**

KATIKA maisha ya binadamu, kuna siku tatu ambazo hukumbukwa daima; siku ya kuzaliwa, ya kuoa au kuolewa na siku ya kifo, na zote hizi huwa na maana kubwa sana.

Siku hizo huendana ama na furaha au majonzi. Siku ya kuzaliwa husherehekewa na wasiozaliwa siku hiyo, huku ya kuoa au kuolewa husherehekewa na anayeoa au kuolewa sambamba na nduguze.

Lakini siku ya kufa kama ilivyo ya kuzaliwa, hushughulisha wafiwa, kwani aliyefariki dunia huwa keshamaliza yake na hana la kufanya wala kuhisi, huwa keshatangulia mbele za haki na kubakiza majonzi kwa waliosalia, hususan wa karibu naye.

Oktoba 25, 2019 ni siku ambayo msichana mdogo Anna Zambi hataisahau maishani mwake. Ni siku aliyopata majonzi yasiyoweza kusahaulika kirahisi wala kuondoka moyoni mwake na hata jamaa zake wa karibu.

Ni siku ambayo akiwa shuleni, shule ya sekondari ya Mtakatifu Teresa wa Calcuta, iliyoko Same, Kilimanjaro, ilitokea ajali mbaya iliyompora wazazi wake na wadogo zake watatu.

Familia hiyo ilikuwa ikitoka Dar es Salaam kwenda Same shuleni kwa Anna, kuhudhuria mahafali ya kidato cha nne ya binti na dada yao huyo, aliyekuwa anajiandaa kufanya mitihani yake ya mwisho.

Akiwa anatarajia familia hiyo kutoka Dar es Salaam kuungana naye katika siku hiyo muhimu katika maisha yake, ndipo Muumba akaamua kuwatwaa wakiwa njiani baada ya gari walilokuwa wakisafiria kusombwa na maji darajani maeneo ya Tanga. Aliwasubiri hakuwaona.

Uongozi wa shule yake ulijulishwa msiba huo, lakini kwa kuzingatia kuwa Anna alikuwa ukingoni akijiandaa kwa mitihani yake ya mwisho, busara ilitumika kumficha, ili amalize mitihani kwani maji yalishamwagika na kama angeambiwa, wangemwaga mengine.

Tukio hili lilinikumbusha mimi kwani nikiwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nikimalizia mitihani yangu ya mwisho, nilifiwa na baba mzazi, lakini kaka yangu aliyekuwa Dar es Salaam alitumia busara hiyo hiyo, kunificha mpaka nilipomaliza mitihani yangu.

Turudi kwa Anna, kutokana na busara ile, marehemu walizikwa na Anna alipomaliza mitihani yake, busara ya uongozi wa shule ile ilitawala tena, kwa kumchukua kimyakimya hadi kwao, ndipo wakamfunulia na kujikuta anashuhudia makaburi ya wazazi na wadogo zake. Bila shaka Mungu alimpa nguvu.

Hata hivyo, kwa uwezo wake Mola, Anna alifaulu mitihani yake ya kidato cha nne kwa kupata daraja la pili na kufanikiwa kuendelea na masomo ya sekondari ya juu katika sekondari ya Canossa, Dar es Salaam, kwa ufadhili maalumu.

Mungu mkubwa, Anna akasoma miaka yake miwili na kumaliza, tena nako huku akifaulu kwa daraja la kwanza kidato cha sita, akijua kuwa sasa ni yatima hana kwingine kwa kushika, ila ni yeye na Mungu wake. Hongera sana Anna.

Jambo la msingi na busara nyingine kubwa iliyomfuata Anna ni kwamba baada ya vifo vya wazazi na wadogo zake, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), alikwenda Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, kuomba kuwa msimamizi wa mirathi ya binti huyo mdogo.

Busara na sheria vikaiongoza Mahakama kuikubalia RITA, hivyo kusimamia nyumba ya familia iliyoko Goba, Dar es Salaam, yenye wapangaji wawili, lakini pia kumfungulia akaunti maalumu CRDB iliyohifadhi fedha za rambirambi, ambazo taarifa zinasema mpaka leo hazijaguswa.

RITA ilimsimamia Anna katika maisha yake yote ya shuleni kwa kumpa matumizi aliyohitaji kutokana na fedha zilizokuwa zikitoka kwenye pango la nyumba na mambo mengine mpaka akafikia alipo hivi sasa.

Anna anataka kusomea sheria ili aje kusaidia wenye matatizo kama yake. Bila shaka ana sifa za kuingia chuo kikuu chochote kwani amefaulu vizuri masomo ya Historia, Kiswahili na Fasihi ya Kiingereza (HKL). Bila shaka ataweza kama alivyoweza huko nyuma na atakuwa mwanasheria. **Inshallah!**

Ombi langu kwa RITA, endeleeni kumshika mkono Anna, kuweni naye katika masomo yake, akifaulu kuwa mwanasheria fanyeni kila linalowezekana awe mwajiriwa wenu, naamini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu atatumikia kwa moyo wake wa shukrani na kwa ufanisi mkubwa.

Pole Anna! Hongera Anna! Mbele kuna nuru. **Alamsiki!**



# SENSA YA WATU NA MAKAZI JUKUMU KUBWA LA FAMILIA

SENSA ya Watu na Makazi ni muhimu sana kwa maendeleo ya taifa. Sensa ya Watu na Makazi nchini itafanyika Agosti 23, mwaka huu. Jambo hili la kitaifa hufanyika kila baada ya miaka 10 na tangu kuasisiwa kwa Muungano wa Tanzania, tayari zimefanyika sensa tano katika miaka ya 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Sensa ya Watu na Makazi ni utaratibu wa kukusanya, kuchambua, kutathmini, kuchapisha na kusambaza takwimu za kidemographia, kiuchumi na kijamii kuhusiana na watu wote na makazi yao katika nchi kwa kipindi maalum.

Kwa lugha nyingine, sensa ni jambo maalum lenye lengo la kupata idadi ya watu wote katika nchi, umri, jinsia, mahali wanapoishi, hali ya elimu na ajira, hali ya vizazi na vifo na hali ya makazi. Kwa mantiki hii, sensa ya watu na makazi si suala la kukaribisha laana na mkosi katika familia, bali la heri na baraka kwa familia, jamii na taifa.

Takwimu hizi za sensa ya watu na makazi zinaweza kuamsha mahitaji halisi ya wananchi yakiwamo makundi maalum yenye uhitaji maalum kwa mfano, watu wenye ulemavu, wanawake, watoto, vijana na wazee. Hii itarahisisha uandaaji wa sera na mipango ya maendeleo kulingana na uhitaji na mazingira yaliyopo.

Kwa muktadha huu, familia zisiwafiche watu wenye ulemavu kutoshiriki katika kuhesabiwa kwani kufanya hivyo ni kinyume cha haki za binadamu na kosa la jinai. Mtu kuwa na ulemavu, hakumwondolei haki zake za kiuchumi na kijamii ikiwa ni pamoja na haki ya kuhesabiwa. Mtu mwenye ulemavu, ni binadamu kama binadamu wengine wenye haki ya kuthaminiwa, kushirikishwa na kuhusishwa masuala yanayohusu maisha yao na taifa lao.

JUKUMU LA FAMILIA

Sensa ya Watu na Makazi ni jukumu la familia kwa kuwa ni mahsusi kwa ajili ya familia, jamii na taifa kwa sababu familia ni serikali ya nyumbani ambayo ni msingi wa jamii na taifa. Bila familia hakuna jamii na taifa. Familia zikiwa imara, kutakuwa na jamii na taifa imara.

Kwa mantiki hiyo, familia ni chimbuko la uhai, shule ya upendo, maadili na uwajibikaji. Familia nyingi zinapitia changamoto mbalimbali za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kimazingira, kisheria, kiteknolojia, kimaendeleo na kiroho. Mabadiliko haya yanaziweka familia nyingi kwenye kipindi kigumu. Utakatifu wa maisha ya familia unazidi kudidimia na kunyauka. Familia nyingi zimepoteza utambulisho na wajibu wa msingi wa kuwa shule ya ukweli, upendo, fadhila na uwajibikaji.

Ni katika muktadha huu, familia zote nchini zinahimizwa kushiriki sensa ya watu na makazi ili serikali iwafahamu watu wake na hali halisi ya mahitaji yao ikiwa ni pamoja na kufahamu umri, jinsi, uhusiano, na hali ya ndoa kwa maendeleo ya familia zenyewe, jamii na taifa. Familia zinapaswa kufanya makazi yao kuwa nyumbani (a home). Nyumbani ni mahali ambapo ndugu na wanafamilia wanapaswa kushangilia ukarimu, wema, furaha, uwazi, uelewano, ukweli, upendo, kukosoana kindugu na kusaidiana.

**MUNGU NI MSINGI**

Sensa ya Watu na Makazi msingi wake ni Mungu mwenyewe. Tangu enzi za manabii na mitume, watu walihesabiwa ili watambulike na kufahamu idadi yao; mahitaji yao halisi kwa ajili ya huduma mbalimbali na maendeleo. Mungu ni Mungu wa mipango na utaratibu.

Mungu alipoumba ulimwengu, aliweka utaratibu wa kutunzwa na kulindwa. Binadamu wote wamepewa jukumu la kutunza, kulinda uumbaji wa Mungu na kuwa chimbuko la maisha yenye furaha.

Hata hivyo, mwanadamu amepoteza wajibu aliokabidhiwa na Mwenyezi Mungu katika kutunza na kustawisha ulimwengu kwa faida yake mwenyewe. Kutokuwajibika ipasavyo na kukosekana kwa uwiano wa kijamii na kiuchumi, kumekuwa chanzo cha mateso na mahangaiko.

Maendeleo ya nchi lengo lake ni kulinda uhai na kustawisha maisha ya watu wake.Uhai na ustawi wa afya zetu ni sehemu ya uumbaji wa Mungu na ajenda ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kwa hiyo, sensa ya watu na makazi itaiwezesha Serikali kupanga mipango ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa ajili ya ustawi wa familia na wananchi wote.

Hali kadhalika, taarifa za idadi ya watu husaidia katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ambayo huakisi matakwa ya watu na uwiano wa mgawanyo wa rasilimali nchini.

Kuhesabiwa ni sehemu ya utambulisho. Kuzaliwa na kuishi tu haitoshi, bali kuishi na kutambulika ni muhimu sana. Watu ili washiriki mema ya nchi yao ni muhimu watambulike. Sensa ya watu na makazi inatoa utambulisho wa pekee kwa familia.

Kwa mantiki hii, familia zote zinaalikwa kuwapo nyumbani siku ya sensa ili kuhesabiwa na kutambulika kwa faida ya familia zenyewe na maendeleo ya taifa, ambapo wewe na mimi ni sehemu yake. Familia katika kaya zote zinao wajibu wa kuhesabiwa na kutengeneza mazingira rafiki ili kufanikisha zoezi hili.

**JUKUMU LA WAZAZI**

Wazazi na walezi ni walimu wa kwanza wa familia. Wazazi na walezi wanao wajibu wa kuelimisha, kuhimiza na kuandaa familia zao kwa ajili ya zoezi la sensa ya watu na makazi. Wazazi wanaopenda familia zao hawatakwepa na kupuuzia wajibu huu. Familia ni kitovu na taasisi ya malezi endelevu.

Katika familia wazazi au walezi wanapaswa kuendelea na jukumu la kuwarithisha watoto wao tunu msingi za matumaini, fadhila, uadilifu na uwajibikaji. Familia za wanadamu zinapotambua mpango wa Mungu maishani mwao, hujitengenezea mazingira salama na kuneemeshwa na Mungu.

Sensa ya watu na makazi ni muhimu kwa maendeleo ya taifa. Ni muhimu wananchi na familia zote kushiriki katika zoezi hili ili taifa lijue idadi ya watu wake na kupanga mipango ya kuweza kuwahudumia vizuri zaidi.

Kwa wale wote waliopewa dhamana ya kusimamia jambo hili, wanapaswa kuhakikisha kazi hii inafanyika kwa ufanisi ili kupata takwimu bora na halisia. Tanzania bora na imara itajengwa na sisi wenyewe kila mmoja wetu atakapotimiza wajibu wake ipasavyo.

**JIANDAE KUHESABIWA**

**[Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

JULAI 17, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili



Ukurasa 13


**Kijivu itakung'arisha**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Namna ya kuosha zulia la ndani



Ukurasa 12

**HARUSI**





# Ondoa mafuta usoni mwako

Ukurasa 14

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | D | U | N | D | A |
| | U | | | E | |
| U | M | A | | R | |
| | A | | B | E | I |
| | Z | | | V | |
| W | A | N | G | A | |

## AMSHA AKILI


NISAIDIE KULIPATA UA LANGU




## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi: CHA, IBA, TANGA, ASALI, ACHIKA, LIMBUA

## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juliana alikuwa akisimuliwa hadithi na bibi yake nyakati za jioni. Bibi alikuwa akimsimulia jinsi zimwi alivyokuwa akiwaadhibu watu wanaokiuka maadili ya jamii yao.

Wakati bibi akisimulia hadithi, Juliana alionekana kuogopa na wakati mwingine alifinya macho kwa hofu.

Baada ya kuona hivyo bibi yake alimuuliza.

**Bibi:** Mjukuu wangu naona unaogopa mazimwi

**Juliana:** Ndio mazimwi nimeyaona kwenye sinema wanakula watu. Tena mwalimu alituambia zimwi likujualo halikuli likakwisha, eti ni kweli?

**Bibi:** Hapana mjukuu wangu, huo ni msemo tu unaomaanisha kwamba mtu anayekufahamu hata akikufanyia ubaya, mwishowe atajirudi na kuona aibu.

**SWALI**

Taja hatua mbalimbali za maisha ya kipepeo

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Si kila unayemuoa ni mkeo, ana mwingine

***KARIBU tena msomaji, bado tunaendelea na simulizi ya kijana Pazi jinsi mke wake Halima alivyomchezea shere na kujikuta akibeba ujauzito wa kijana aliyemkataa awali huko kijijini kwao. Kumbuka, siyo kila unayemuoa ni mkeo au mumeo. Alishakuwapo mwingine.***

Bibie Halima baada ya kudumu kwenye ndoa miezi sita na kujiona hapati ujauzito, alileta kiburi chini kwa chini. Hata mumewe alipohamishwa kikazi kwenda Hoteli ya Mikumi yeye alikataa na kutaka arudishwe kwao.

Kijana Pazi bila kujua hili wala lile akamrudisha kwa wazazi ili akaendelee na kazi yake ya hoteli. Alipofika kwao aliwaeleza wazazi wake aliyokuwa anapitia na kuwaambia kuwa amekuja na anataka apewe talaka.

Kumbe ulikuwa mpango mzima wa kijana aliyemchumbia awali lakini akamkataa na sasa amepania piga ua lazima amtwae kuwa mke wake. Alichofanya ni kumpa ujauzito irahisishe kuwa karibu naye.

Wiki iliyopita tuliona mchakato wa kijana huyo wa kijijini wa kutoa posa ulivyogonga mwamba, huku baba mzazi wa binti akikataa pesa na barua ya posa akiichoma moto.

> **“Mzee akambana mama mbona huyu mtoto anaonekana kama kajifunga? Mama akajibu ndiyo mzee, kasema mwenyewe. Baba akamfukuza yule binti aende kwa huyo aliyempa mimba.**

Kijana huyo akabadili mbinu akawatuma wazee wambembeleze baba apokee barua ya uchumba wa bintiye, yule mzee akakataa kabisa. Baada ya miezi miwili mzee akamwona binti amebadilika kumbe ni mjamzito!

Mzee akambana mama mbona huyu mtoto anaonekana kama kajifunga? Mama akajibu ndiyo mzee, kasema mwenyewe. Baba akamfukuza yule binti aende kwa huyo aliyempa mimba. Binti ikabidi atekeleze agizo hilo.

Ilikuwa siri lakini sasa hadharani, habari zikatapakaa kijijini hadi wakwe zake wakajua, na Pazi mume wa ndoa akapata habari. Pazi kusikia hivyo akainua mikono juu akasema; Asante Mungu.

Baada ya miezi tisa binti akajifungua watoto mapacha. Baada ya miaka minane ndani hakukaliki kila siku ngumi mpaka binti kavunjwa kidole. Kijana akawekwa rumande siku mbili na kutolewa na wazazi wa yule binti. Majirani wakiulizwa wanasema hayo ndiyo maisha aliyoyachagua!

Mume wa pili wa Halima akapeleka talaka, bibi hajui kusoma akampa mjukuu wake na alipoisoma ni talaka tatu. Bibi akashangaa, hee, kulikoni!

Bi. Halima kupokea talaka akataka kupata mawasiliano ya Pazi. Akaambiwa labda aende hoteli ya New Afrika wao watajua aliko. Kesho yake akaenda akapokewa pale hotelini. Akaulizwa tukuhudumie nini, akajibu hapana, namuulizia tu Pazi kama mnajua alipo.

Wakamwambia Pazi yuko Kunduch Beach Hotel na kama unataka kwenda lipo gari la ‘staff’ tutakuombea lifti. Gari ikafika akapelekwa Kunduchi. Pazi akajulishwa yuko mgeni wake mapokezi. Pazi kutokea tu na kumuona mkewe wa kwanza akamuuliza kulikoni. Binti akaanza kulia.

Kabla ya kuhamishwa toka Mikumi kuja Kunduchi, ilibidi kijana aoe mke mwingine aitwaye Salha. Akapewa cheo cha meneja wa vyakula na vinywaji. Pazi akaanza kumuuliza mkewe wa kwanza, mbona umekuja huku? Akaanza kulia Pazi akapata mshangao. Akamwita kwa jina la Halima, una nini?

Halima akatoa karatasi kumpa Pazi na alipoisoma kumbe ni talaka. Pazi akamuuliza mimi nifanyeje? Nakuomba turudiane. Pazi akamjibu itakuwa ngumu kwani nimeshaoa na nina watoto wawili, siwezi kuwa na mitala!

Hapo akamzidishia kilio kama mtu kafiwa na mtoto wa kwanza. Ikabidi watoke pale mapokezi wakae mbali kidogo na wateja kwani ulikuwa muda wa chakula.

Pazi akamtuma mhudumu amletee chakula na kinywaji. Bibie akala chakula kwa shida kwa sababu alikuwa na kwikwi ya kulia. Alipomaliza kula akaitwa mhudumu ampeleke kwa matroni kule hosteli akapumzike.

Pazi akarudi nyumbani na mawazo tele hadi mkewe akamshtukia ikabidi amuulize, mbona hauko sawa leo? Pazi akaduwaa, akamuuliza tena kuna nini? Akasema. Aah, kuna watu wengine wanapenda kuvuruga maisha ya watu. Mke akauliza tena, si useme tu?

Pazi akaanza kutoa machozi kwa mbali kama vile mtu kaletewa habari ya msiba. Kwa wanaume kulia kama mwanamke ni aghalabu sana. Muda mfupi baada ya kutulia akaanza kumwelezea yote yaliyojiri. Mke akamwuliza kwa hiyo umechukua uamuzi gani?

***Hah! Itabidi arudi nyumbani, kivipi? Wanandoa hawa wawili hakuna aliyepata usingizi. Je, nini kiliendelea baada ya taarifa hizo. Fuatilia sehemu ya mwisho ya simulizi hii. Je, una maoni, Kisa cha kimaisha. Tuma ujumbe kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Mashine hizi uwanja wa ndege ziboreshwe

UNAPOSAFIRI kwa ndege kwenda nje ya Dar es Salaam au unaporejea ni lazima mizigo yako ikaguliwe kwa kupitishwa kwenye mashine maalum iliyopo kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA).

Baada ya kuchukua mizigo wako, moja kwa moja unakwenda kuweka kwenye mashine maalum, ambayo lazima upitishe kila ulichonacho ikiwamo kompyuta mpakato (laptop).

Ziko aina nyingi za mashine hizi zinazoweza kutunza mizigo ya abiria wanaotoka nje ya mkoa na nchi lengo likiwa kuzuia visivyoruhusiwa kuingia nchini na ndivyo inavyofanyika kwenye mipaka yote nchini.

Ziko pia mashine ambazo mzigo ukishapita unaupokea upande wa pili na kutokana na kasi ya mashine hadi unafika mzigo wako umeshasogezwa mbele zaidi ambako hutegemea aina ya mashine.

Mashine ambazo zinaacha mizigo yenye kuvunjika salama ni ambazo mbele zina meza ambayo inawezesha mizigo kukaa vizuri bila uharibifu.

Tatizo kubwa ni kwa zile ambazo mzigo ukishatoka kwenye mashine unaanguka kwa mteremko mkali ambao hufuatiwa na mizigo mingine ambayo huangukiwa juu yake na kusababisha usumbufu na uharibifu.

Wako baadhi ya wasafiri kwa mashine hizo wameharibu kompyuta zao ambazo ziliangukiwa na mizigo mingine zikavunjika au vifaa vingine ambavyo lazima uvitoe kwenye pochi au begi na kuweka sehemu husika.

Pia wapo wanaokuwa na ndoo za kitoweo, mabegi makubwa ambao panapokuwa na wasafiri wengi yaani ndege imeshusha abiria wengi kwa wakati mmoja, ni lazima kila mmoja aweke mizigo yake kwenye mashine husika.

Ni muhimu kuhakikisha usalama wa mizigo ya watu kwa kubadilisha vifaa vya kupokea kwa kuweka meza mbele yake kuliko kuacha mizigo kuangukiana na kusababisha uharibifu.

Inaweza isionekane tatizo kubwa sana kwa kuwa huenda watu hawalalamiki au wanapoondoka eneo la uwanja ndipo wanagundua uharibifu huo lakini kimsingi ni tatizo kubwa linalokera wengi katika uwanja huo hasa ‘Terminal II’.

Unapotembea duniani mashine za kuchagua mizigo ni ambazo zinatunza mizigo ya wasafiri, nasi tuige hilo kwa manufaa ya kuzidi kutangaza matumizi ya uwanja wetu zaidi.

Mathalani, wageni wengi wanaotoka mikoa mbalimbali wanarudi Dar es Salaam, ni lazima watumie uwanja huo kama wamebeba vifaa vyao vinavyoweza kuvunjika huenda wamepata hasara na kuona uwanja huo siyo salama kwao.

> **“Mtu anapoharibikiwa na kompyuta, simu au kamera kwa sababu ya utaratibu wa mashine husika inakuwa ni hasara kwake na taifa kwa ujumla.**

Nawaza kwa sauti kwamba uwanja huo unaweza kuonekana kikwazo, hivyo jambo linaloweza kuboreshwa ni muhimu likafanyika ili kuhakikisha mizigo ya wasafiri inakuwa salama hadi anapotoka nje ya uwanja.

Mtu anapoharibikiwa na kompyuta, simu au kamera kwa sababu ya utaratibu wa mashine husika inakuwa ni hasara kwake na taifa kwa ujumla.

Lakini wanaosafirisha kitoweo wakati mwingine ndoo zinapoanguka chini kwa mteremko mkali kuna uwezekano wa kupasuka, hali itakayompa shida mmiliki.

# HARUSI



Julai 9 mwaka huu, Juma Kalemera aliaga ukapera na kufunga ndoa na Juliana Mwendakazi, huko Ukonga na kufuatiwa na sherehe iliyofanyika katika ukumbi wa Mawela, Sinza Dar es Salaam. Mungu awatangulie katika ndoa yao.











# MITINDO














## Kijivu itakung'arisha

KAMA hujawahi kutoka ukiwa na furaha, basi jaribu kupangilia mavazi yako kwa rangi ya kupendeza na yenye kuvutia zaidi.

Wataalamu wa mavazi wanasema nguo za rangi ya kijivu na nyeupe, zinampa mtu mwonekano unaong'aa na wenye hadhi ya kipekee.


Rangi ya kijivu ni pendekezo sahihi kwa wale wanaotaka kutoka kwa ajili ya matembezi au kwenda kuonana na rafiki katika sehemu tulivu.

Inapendeza zaidi kama ukivaa shati au fulana ya mikono mirefu na suruali nyeupe ambayo inaongeza umaridadi kwa mhusika.

Hata hivyo, nguo ya rangi ya kijivu haichagui aina ya suruali kama vile 'jeans', kadeti au ya kitambaa hata ikiwa na rangi tofauti.

Kama una mapenzi ya kuvaa tai, kofia au skafu, hautakuwa na tatizo kwani aina hizo za nguo zitakupa matokeo mazuri.

Miguuni hautakosea kama utapigilia viatu vya kisasa vya ngozi, raba, sendo au buti.



UREMBO

# Ondoa mafuta usoni mwako

WAPO baadhi ya watu nyuso zao zinameremeta muda wote kwa sababu ya kujaa mafuta.

Watu wa aina hii wamekuwa wakishauriwa kutumia aina ya mafuta ambayo yanakausha mafuta ili kuwaweka sawa.

Tuungane katika kuangalia njia sahihi za asili za kukusaidia kuweka uso wako wenye mafuta sawa.

**Mafuta ya Nazi**

Mafuta ya nazi ndio dawa tosha, unaweza ukashangaa kwa kudhani kwamba utazidisha tatizo, la hasha.

Mafuta ya nazi yanakinga ngozi na bakteria, mwanga wa jua pia ukipaka usoni muda wote unakuwa mkavu.


Mafuta yasiyochanganywa na kitu chochote ndio salama kwa afya ya ngozi yako.

**Usijishike shike uso**

Mafuta mengi yanasababishwa pia na ngozi iliyokufa, ukiwa una shika shika uso unaongeza uchafu na bakteria.

Endapo unahisi mafuta yamezidi basi tumia karatasi laini jifute utosini, pua na kidevuni na usijishike uso wako.

Endelea kuzingatia hayo na utaona matokeo makubwa sana na kujipenda kwa rangi nzuri na sura utakayokuwa nayo.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Tengeneza keki ya chocolate nyumbani

KEKI ya chocolate inapendwa na watu wengi. Baadhi hununua madukani au kuweka oda kwa ajili ya kutengenezewa kwa gharama kubwa.

Idadi kubwa wamezoea kula keki hizi kwa kuletewa zawadi au kununua wenyewe, wachache sana wanaotengeneza nyumbani.

Leo tutakufanya uwe mdau wa keki kwa kuipika mwenyewe nyumbani kwa njia rahisi kabisa na salama.

**MAHITAJI**

Mayai sita, blueband ya kupima robo kilo, unga wa ngano robo kilo, sukari robo kilo, Cocoa gram 40 na Baking powder kijiko kimoja cha chakula.

**MATAYARISHO**

Kama unatumia jiko la mkaa, washa jiko liendelee kushika pole pole.

Tayarisha sufuria yako ya kuokea keki kwa kuweka karatasi chini na kupaka siagi ili iwe rahisi keki kutoka itakapoiva.

Weka mayai, sukari na blueband kwenye blender ublend kwa takriban dakika kumi.



Mimina mchanganyiko kwenye bakuli, gawanya unga mafungu matatu.

Weka unga kwenye mchanganyiko fungu baada ya fungu huku ukichekecha kisha ukoroge vizuri.

Endelea kufanya hivyo mpaka mafungu yaishe. Kuchekecha unga inasaidia mavumbi ya unga kubaki juu. Na kuweka unga fungu baada ya fungu inasaidia unga kukorogeka vizuri zaidi.

Weka baking powder uchanganye vizuri na weka cocoa pia uchanganye vizuri.

Mimina kwenye sufuria na uoke kwa kutumia jiko la mkaa. Ifunike keki yako na uweke mkaa juu na kwenye jiko ubakishe kidogo.

Hakikisha juu huweki mkaa mwingi sana ili keki yako isiungue. (Unaweza ukatumia oven) na oka kwa dakika 40 hadi 50.

Weka kijiti ndani na kikitoka kikavu basi keki ipo tayari kwa kuliwa na kinywaji chochote utakachopendelea.

# MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



## Namna ya kuosha zulia la ndani



KATIKA maeneo ya mjini watu wanapenda kuosha mazulia bafuni ili kupunguza uwezekano wa kuchafuka.

Lakini hata nje ya nyumba ni eneo salama kwa kazi ya uoshaji wa zulia kama utachukua tahadhari zote za kuchafuka na vumbi wakati wa kuanika.

Ni rahisi sana kuosha zulia bafuni na hata nje kama utafuata njia zifuatazo.

**1:** Kabla ya kuanza mchakato kusafisha zulia, kwanza angalia usafi wa maji na kuondoa vitu vigeni kuzunguka eneo husika. Andaa sehemu ambayo utaning'iniza kapeti wakati unasugua kwa kutumia brashi.

**2:** Kuwa makini! kabla ya kuanza kuosha zulia nyumbani ni lazima kuchagua aina ya sabuni na eneo la kukaushia.

**3:** Osha kwa kutumia sabuni na maji ya kutosha, huku ukisugua kwa brashi ili uchafu utoke. Hakikisha unagusa kila kona ya zulia ili uchafu usibaki.

**4:**Kama kuna hali ya joto kukausha mazulia inakuwa haraka, unahitaji kufungua madirisha, hivyo kutoa hewa ya kutosha. Ni muhimu kukausha sehemu isiyo na jua kali ili kudhibiti ubora wa rangi.

# Namna ya kusafisha dirisha

DIRISHA ni moja ya vitu vinavyochangia kung`arisha nyumba. Lakini, ili dirisha liendelee kuwa bora na kung`arisha nyumba lazima lisafishwe.

Endapo usipoweka kipaumbele katika jambo hilo usishangae kuona mvuto wa nyumba yako kuanza kufifia kidogokidogo na mwisho wake ukaichukia nyumba kabisa. Usafishaji wa dirisha ni lazima uwe na muda maalum ambao hakuna jua kali.

Na hiyo ni kwa sababu unaposafisha wakati wa jua kali, maji unayomimina katika dirisha lako hukaushwa hata kabla ya kupitisha sponji na hivyo itakuchukua muda mwingi na pia haliwezi kung`aa vizuri na huacha ukungu.

Wakati unasafisha unatakiwa uwe pia na dawa maalum au kama unatumia maji si vibaya ukadondoshea kidogo vitone hata viwili vya maji spesho yenye mchanganyiko wa limao, maarufu kama 'vinegar'.

Baada ya hapo unalowanisha 'sponji' yako au kitambaa laini kwa kuchovya kwenye maji hayo na kuanza kusafisha katika dirisha lako.

Hakikisha unasafisha kuanzia juu kushuka chini, ili uchafu wote utiririkie huko kwa sababu kufanya hivyo kutakuhakikishia kuwa hakuna uchafu utakaodondokea kwenye sehemu ambayo umeshasafisha tayari.

Kama eneo la dirisha unalotaka kusafisha ni chafu sana au kuna vumbi jingi au utando wa buibui, futa kwanza kwa kitambaa kikavu kabla ya kusafisha na maji.

Uwe makini kuchunguza uchafu ulioko kwenye kona za madirisha yako.

Pia epuka sana kuweka maji mengi kwenye sponji au kitambaa chako unachotumia kusafishia ili yasimiminikie chini sehemu ambayo siyo ya dirisha iwe ukutani ama sehemu nyingine isiyohusika.



Hakikisha unasuuza na kukausha dirisha lako kwa kutumia kitambaa kikavu na laini na baada ya hapo rudia tena kwa ajili ya kuling`arisha.


Kama utakuwa na dawa maalum ya kusafishia itapendeza zaidi kuipulizia kidogo katika dirisha lako huku ukifuta kwa kutumia kitambaa cha pamba ambacho hakitoi nyuzi.

Hakikisha dawa unayotumia kusafishia ni ile ambayo haiwezi kuharibu au kupausha mbao za dirisha lako.

Kama dirisha lako ni la kioo, hakikisha sponji au kitaamba ulichotumia kusafishia kioo ni tofauti na kile unachosafishia kwenye fremu ama kona za dirisha lako.

Katika maeneo ya fremu na kona, safisha kwa kutumia kitambaa kigumu zaidi ambacho kitabeba uchafu wote kwa sababu eneo hilo huhifadhi uchafu mwingi.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA 2022
NA MUHIDINI MSAMBA
0656 122770 SMS
...HADUBINI...
HE SURA KAMA UMEZURUMIWA CHENJI NA KONDA WA DALADALA
HIYO KAZI YA UTABIRI UMEANZA LINI?
KASHESHE
JANA MIMI NA MUME WANGU TULIENDA KUPIMA UKIMWI MAJIBU YAMEONYESHA TUPO SAFI
HEHEHEHE... HALOOO HALOO MIMI MZIMA WA AFYA SIAMINI!
INAMAANA TUMEKUPIMIA!?
HABARI NDIYO HIYO
KITAA CHA KWETU
KILIKIZO KAMA HIKI KIPINDI KILE NILIKUWA NAZOLEWA KWENYE MITALO YA MAJI MACHAFU KWA ULEVI, KWELI MAISHA YANABADILIKA
NIMEKAA HAPA ZAIDI YA MASAA MAWILI NAMSUBIRIA MUUZA HAYA MAYAI,KAENDA KUNITAFUTIA CHENJI YA ELFU KUMI
POLE MKUU USHA PIGWA
NDANI YA KIBASI
WEWE DEREVA VIPI HUO MWENDO GANI
MWENDO HADI TUNAPIGA CHIAZI NA MAWINGU
KAMA HAUNA FAMILIA WENZIO TUNAFAMILIA
HUYU ATAKUWA HANA FAMILIA INAYO MTEGEMEA
ATAKUWA ANAISHI GETO MSOSI KWA MAMANTILIE, NDIYO MAANA ANA ROHO NGUMU KAMA CHUMA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...CHUMVI HAIWEZI KUWA SUKARI...

# Russia yashambulia vikali Odesa

**KYIV,** UKRAINE

JANA anga la mji wa Odesa nchini Ukraine, lilitawaliwa na moshi mzito angani baada ya makombora mawili kushambulia mapema asubuhi.

Mashambulizi hayo yamethibitishwa na msemaji wa utawala wa jeshi wa jimbo hilo, Sergei Bratchuk, na makamanda wawili wa jeshi la Ukraine.

Waokoaji walianza kufanya kazi katika eneo la tukio hilo, lakini hakuna taarifa rasmi kuhusu madhara yaliyopatikana.

"Kulikuwa na mashambulizi katika ghala la biashara na viwanda, kulikuwa na moto mkubwa. Namshukuru Mungu hakuna majeruhi. Na kuna kitu muhimu hapa nilishotaka kusema asubuhi walinzi wa ghala walifuata kanuni za mienendo wakati wa uvamizi wa anga," alisema Bratchuk.

Mashambulizi ya makombora ya masafa marefu ya Russia yalifanyika katika mji wa Chuguev uliopo katika jimbo la Kharkiv na kuharibu shule, majengo ya kibiashara na makazi kadhaa ya watu.

Watu watatu wameripotiwa kufariki na wengine wengi kujeruhiwa na kwa sasa wamelazwa hospitali, limeandika shirika hilo likinukuu mtawala wa jimbo hilo Oleg Sinegubov.

**CHUGUEV HAKUKALIKI**

Takriban watu watatu wameuawa katika eneo la Chuguev ambako Russia ilipiga kwa kombora jana asubuhi.

Wakati huo huo idadi ya watu waliokufa kutokana na shambulio la Warussia la roketi katika mji wa Vinnitsa, imepanda na kufikia hadi watu 24.

Mtu mmoja aliyekuwa amelazwa kutokana na shambulio hilo amefariki kutokana na majeraha, alisema mtawala wa jimbo la Odessa, Sergei Borzov.

Jumla ya watu waliofariki hadi sasa ni 24, huku wengine 68 waliojeruhiwa wakiendelea kuuguza majeraha, wakiwemo watoto wanne.

**BIDEN ATARAJIA MAFUTA ZAIDI SAUDI ARABIA**

Rais wa Marekani, Joe Biden, alikutana na viongozi wa Kiarabu nchini Saudi Arabia jana, wakati akijaribu kutafuta ushawishi wa kuongeza uzalishaji wa mafuta.

Kiongozi huyo aliangazia mkutano wa kilele uliopangwa na nchi sita za Ghuba na Misri, Jordan na Iraq huku akipuuza kukutana na Mwanamfalme wa Saudia Mohammed bin Salman.

Biden alikuwa ameahidi kuitenga Saudi Arabia katika jukwaa la kimataifa kutokana na mauaji ya mwanahabari Jamal Khashoggi mwaka wa 2018, yaliyofanywa na maofisa wa Saudia, lakini aliamua kulegeza kamba akisema maslahi ya Marekani yanataka kurekebishwa, sio mpasuko.

Biden anahitaji msaada wa Saudia katika wakati ambao bei za mafuta ghafi zinazidi kupaa juu na matatizo mengine yanayohusiana na mzozo wa Russia na Ukraine.

Rais wa Marekani atafanya mazungumzo ya pande mbili na viongozi wa Misri, Umoja wa Falme za Kiarabu na Iraq kabla ya kushiriki katika mkutano huo.

Kiongozi huyo atajadili usambazaji wa nishati na wazalishaji wa mafuta wa Ghuba, lakini Marekani ilisema haitarajii Saudi Arabia, mwanachama wa nguvu wa OPEC kuongeza uzalishaji mafuta mara moja.

**BBC**



Picha iliyotolewa na Mamlaka ya Hifadhi ya Thailand ikimuonyesha mtoto wa tembo akiokolewa na kijiko baada ya kukwama ndani ya shimo lenye tope. Mama wa tembo huyo alizimia kutokana na kuwa na msongo wa mawazo kutokana na mtoto wake kushindwa kumuokoa.
**PICHA : AFP**

# Wabunge Sri Lanka kumtafuta rais mpya

**COLOMBO,** SRI LANKA

WABUNGE wa Sri Lanka wameanza kikao cha kuanza mchakato wa kumchagua kiongozi mpya ili kukamilisha muhula wa rais wa zamani Gotabaya Rajapaksa.

Rajapaksa aliikimbia nchi hiyo na kisha kujiuzulu kufuatia shinikizo la maandamano ya umma.

Spika wa Bunge la Sri Lanka, Mahinda Yapa Abeywardana, alisema mchakato huo utafanyika kwa utulivu na uwazi na inatarajiwa rais mpya atapatikana katika muda wa wiki moja inayokuja. Kulikuwa na ulinzi mkali kuzunguka majengo ya bunge mjini Colombo wakati wabunge walipohudhuria kikao cha kutafuta muongozo wa utaratibu wa uchaguzi wa rais mpya kabla ya kupiga kura siku ya Jumatano inayokuja. Juzi Waziri Mkuu wa utawala wa Rajapaska, Ranil Wickremesinghe aliapishwa kuwa kiongozi wa mpito na atabakia madarakani hadi pale bunge litakapokamilisha mchakato wa kumpata rais mpya. **DW**

## Kenya, Somalia zatangaza makubaliano

**NAIROBI,** KENYA

RAIS wa Kenya Uhuru Kenyatta, amekutana na kiongozi wa Somalia Hassan Sheikh Mohamud mjini Nairobi na kutangaza mabadiliko kadhaa ya kisera yanayolenga kurejesha uhusiano na kupunguza mivutano ya kidiplomasia.

Taarifa ya pamoja iliyotolewa na wizara za mambo ya kigeni za mataifa yote mawili zilisema Kenyatta na Sheikh Mohamud walikubaliana kuondolewa kwa vizuizi vya mipakani na kurejea kwa biashara ya bidhaa muhimu ikiwemo usafirishaji mirungi.

Kadhalika viongozi hao wameridhia kurejea kwa safari za ndege za shirika la Kenya Airways mjini Mogadishu na kuondoa ulazima wa viza kwa wanadiplomasia wa pande hizo mbili wanapotembeleana.

Kwa miaka kadhaa mahusiano kati ya Kenya na Somalia yametetereka kutokana na misuguano iliyochochewa kwa sehemu kubwa na mzozo kuhusu eneo la bahari ya Hindi ambalo mataifa yote mawili yanadai umiliki wake.

## Mashambulizi ya Israel ukanda wa Gaza

**TEL AVIV,** ISRAEL

ISRAEL imelishambulia eneo la kijeshi linalomilikiwa na kundi la Hamas kwenye Ukanda wa Gaza kujibu kile nchi hiyo inadai ilitupiwa maroketi kutoka Gaza.

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana ndege za kivita zikilenga kituo hicho kinachoaminika kutumiwa na kundi la Hamas kuunda maroketi .

Shambulizi hilo lilifanywa saa chache baada ya makombora mawili kurushwa kutoka Gaza kuelekea Israel.

Hata hivyo makombora hayo yalidunguliwa na mifumo ya ulinzi ya Israel na taarifa zinasema hakuna mtu aliyejeruhiwa au uharibifu uliotokea.

Hadi sasa bado hakuna kundi la Kipalestina lililodai kuhusika na urushaji huo wa maroketi, lakini Israel imelibebesha lawama kundi la wanamgambo wa Hamas wanaotawala Ukanda wa Gaza.

**DW**

MAKALA

# AFRIKA TUTAKWISHA



Na Magabilo Masambu - 0689157789

SIKU za karibuni tumekuwa na msamiati unaitwa "matokeo makubwa sasa". Pamekuwapo na juhudi za makusudi kuhakikisha kila jambo linapata matokeo makubwa. Jambo hili likanikumbusha wakati fulani nilipokuwa shule ya bweni pale Ifunda, siku za kula wali tulikuwa tunaulizwa mnataka 'quantity' au 'quality'?

Kwa kuuliza hivyo walikuwa na maana kwamba kama tunataka 'quantity' tupikiwe aina fulani ya mchele unaitwa 'Kitumbo'. Ukipikwa kidogo tu unavimba na kujaa sufuria lakini unafanana na kande na kama tunataka 'quality' tupikiwe mchele aina ya supa unaonukia lakini tutapewa kidogo maana hauvimbi.

Sasa kwa sababu tulitaka kushiba tu na si kula kitu bora, tukawa tunaitikia tunataka 'quantity'. Tukishasema hivyo, mchele aina ya Kitumbo unachukuliwa na kupikwa. Sifa kubwa ya mchele huo haukolei mafuta na mbaya zaidi hauna ladha yoyote wakati unakula. Ni kama unatafuna mahindi makavu yaliyochemshwa hapa Arusha yanaitwa "makukulu". Kwa hiyo tukawa tunafurahia kwa sababu tuliwekewa mwingi kwenye sahani japo hatukuwa tunaufurahia.

Tumekuwa na tabia ya kupenda wingi katika maeneo mbalimbali bila kujali ubora.Tukaanza kwenye elimu mtazamo wetu ukawa ni kupeleka vijana wengi sana sekondari huku tukidhani kwamba tutakuwa tumetatua changamoto za elimu, msisitizo mkubwa ukawa matokeo makubwa sasa bila kutazama zaidi ubora wa matokeo hayo si kwa maana ya ufaulu wake, lakini kwa maana ya maarifa na ujuzi utakaowafanya watu wajiajiri. Katika hilo tulifanikiwa na sasa leo shule zote nchini zinashindana juu ya matokeo ya mitihani si juu ya ujuzi.

Baadaye tukahamia kwenye eneo la kilimo na hapa hali ni mbaya zaidi. Sina hakika kama wote tumeona kama ninavyotazama. Kabla ya matokeo makubwa sasa, tulikuwa na mbegu zetu za asili za mazao, matunda, mboga na kadhalika. Mara tukaambiwa tunatakiwa kuzalisha kwa wingi na kwamba hizi za asili zinafanya tupate mavuno kidogo.

Tukaletewa mbegu tunazoambiwa ni za kisasa na kwamba zinazaa maradufu lakini tukaambiwa hizi mbegu hazipandwi hivi hivi lazima ziambatane na mambo mengine kama vile mbolea za kupandia na kukuzia. Lakini pia eti huwezi kuvuna kama hutapiga dawa za wadudu.

Hili la dawa likanikumbusha nyakati zile nilipokuwa kijijini pale Bulenda Bufwe, kwamba zao pekee lililokuwa likipigwa dawa ni pamba na ile dawa ilikuwa ikitokea pengine ng'ombe au mbuzi akala majani ya pamba muda mfupi baada ya kupuliza alikuwa anakufa. Sasa nikajiuliza hivi huu utamaduni wa kupuliza dawa katika mazao tunayotumia kama chakula ni kweli kwamba umefanyika utafiti wa kutosha na kuleta majibu kwamba dawa hizo hazina athari zozote kwa afya zetu?

Ikanikumbusha zaidi kwamba mbona zamani tulikuwa tukivuna mahindi yetu haya ya kienyeji tulikuwa tunachagua mahindi ya mbegu tunatundika kwenye mti au jikoni mpaka yanafika msimu wa pili bila kuoza? Leo ukishamaliza kuvuna mahindi bado unaambiwa weka dawa ili yasiliwe na wadudu yaani mahindi ambayo wadudu hawali ni salama kwa binadamu.

Lakini nikakumbuka jambo linguine. Mwaka 1995 babu yangu alikuwa mwenyekiti wa serikali ya kijiji wakati ule Kanda ya Ziwa kulikuwa na uhalifu wa kutumia sumu kuvua samaki. Wale walliokuwa wakikamatwa pamoja na mitubwi yao walikuwa wakiadhibiwa kwetu ikiwa ni pamoja na kutaifisha mitubwi na boti zao.

Haya yalifanyika kwa ajili ya kulinda afya za walaji. Sisi walewale tuliopinga walaji kula sumu kwenye samaki tumeona ni halali tule sumu kwenye mahindi, kabichi, mboga, matunda na kadhalika tutakuwa salama kweli?

Mimi si daktari na siwezi kuthibitisha hili lakini utafiti ukiendelea kubaini chanzo cha ongezeko kubwa la wagonjwa wa saratani na kadhalika kwa sababu mwaka 2006 nilipata nafasi ya kutembelea Taasisi ya Saratani ya Ocean Road wakati ule wagonjwa walikuwa wachache sana. Sijapata nafasi ya kurudi pale siku za hivi karibuni, lakini kwa vyovyote vile idadi yao itakuwa imeongezeka maradufu au zaidi. Ni kweli kwamba inawezekana saratani hizo zinatokana na sababu mbalimbali, lakini mojawapo yaweza kuwa matumizi ya sumu katika vyakula tunavyotumia kuanzia kwenye wale samaki wenye sumu waliokuwa wakikamatwa wakati ule.

Jambo baya zaidi ni kwamba huku kuhitaji matokeo makubwa sasa yameharibu kabisa ardhi yetu kiasi kwamba imekuwa kama mwanamume asiye na nguvu za kiume ambaye anahitaji viagra ili kukamilisha utaratibu wake. Leo huwezi kulima bila kutumia mbolea wala dawa ukavuna. Ni sehemu chache tu huko vijijini zimebaki lakini kwa kweli hali ni mbaya.

Najaribu kuwaza miaka 20 mbele uzalishaji wetu katika eneo la kilimo utakuwaje? Je, ni mpango mkakati uliojificha kwenye matokeo makubwa sasa ili baadaye tusizalishe chochote na tutegemee misaada kutoka mahali fulani? Tusipokuwa makini tutakuwa tegemezi tangu kwenye elimu mpaka kwenye uzalishaji wa chakula chetu wenyewe.

Kweli waungwana tunasomesha wataalamu wetu wa kilimo wanaokwenda kuuwa mbegu zetu za asili kwa kisingizio cha mavuno mengi? Je, tuna tofauti gani na wale waliokuwa wanatumia sumu kuua samaki wengi kwa wakati mmoja lakini madhara yake yakiwa makubwa? Leo samaki wameisha lakini magonjwa kwa watu yanaongezeka.

Mwisho, niombe iundwe timu maalumu kuchunguza madhara yatokanayo na matumizi ya vyakula vinavyopuliziwa dawa maana kuna siku nikiwa sokoni nilisikia mama mmoja anasema anatafuta mboga iliyoliwa na wadudu maana haina sumu. Maana ya kauli hiyo ni kwamba tunakula sumu za kutosha na mwisho wa siku Afrika tutakwisha.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# 'Nimemkaribisha Nyoka' Tancut Almasi, mama aliyemkaribisha 'mke mwenzake'



Na Adam Fungamwango

KWENYE maisha ya ndoa kuna mambo mengi sana, hivyo yeyote anayetaka kuingia huko anapaswa ayafahamu ili kukabiliana nayo. Ni lazima yeyote anayetaka kwenda sehemu kujua angalau uzuri na changamoto za huko anakokwenda ili aanze mchakato wa kukabiliana nazo.

Kwenda sehemu kwa kushtukiza itakupata changamoto ambayo hukuitarajia ni jambo linalosababisha mtu kuitatua kwa mihemko, badala ya kutumia busara, hekima na taratibu.

Kwa miaka ya karibuni, tumeona nyimbo nyingi za muziki wa kisasa zikizungumzia mapenzi tu. "Nakupenda, nakupenda, wewe ni wangu, tufunge ndoa." Ni kweli lengo la ndoa ni kupendana na kuwa na furaha, utulivu na amani.

Lakini hata wanaofungisha ndoa huwa wanawauliza wanaofunga "Mtapendana kwa shida na raha?"

Hii inaonyesha watu wa dini pia wanajua kuwa ndoa pamoja na kwamba ni jambo takatifu kwa sababu wanaoishi ni watu wawili, waliolelewa katika mazingira tofauti ni lazima kuna sehemu watakwaruzana, ingawa inakuwa kwa muda fulani fulani.

Mara nyingi uvumilivu ndio unaotakiwa ili kuvuka hapo. Ukiona wanandoa wamekaa miaka 30 mpaka 50 ya ndoa yao, si kwamba ilikuwa na raha tu. Walipitia changamoto nyingi sana lakini walikuwa wavumilivu, wakakaa chini kuyasuluhisha na wakavuka salama.

Hizo changamoto ndizo wasanii wa kizazi cha sasa huwa hawataki kuziimba ili kuwaelimisha na kuwakumbusha vijana wanaotaka kuingia kwenye ndoa kuna hili na hili. Inatakiwa mtu anapopata umri wa kuoa aoe, lakini ni lazima kichwa kiwe kimetulia na ujue unakwenda kufanya nini.

Wengi waliodhania ukioa tu au kuolewa basi unakuwa kama dunia yote ni yako hakuna changamoto zozote utakazokutana nazo, ndio wanaokuwa na kipindi kifupi tu kwenye ndoa, kabla ya kunyoosha mikono juu, yaani kuachana.

Vijana Jazz Band waliimba wimbo mmoja uitwao 'Tamu na Chungu ya Ndoa'. Una maneno yafuatayo;-

*"Ndoa ina tamu na chungu ulielewe hilo mpenzi wangu wewe. Tutakapooana tutafanya sherehe nyingi, lakini kumbuka maisha ya ndoa yana taabu na raha, aa yaya, tusiyafuate maneno ya pembeni, yataharibu bure ndoa yako.*

Uvumilivu kwenye ndoa ni muhimu, hakuna ndoa inayokosa misukosuko."

Wimbo huu umemaliza kila kitu. Ila sasa nataka nikupe kisa kimoja kilichotokea kwenye ndoa moja hivi ambacho kimesimuliwa na bendi ya Tancut Almasi Orchestra iliyokuwa na maskani yake Iringa.

Wimbo huo ulitungwa na Kyanga Songa unaitwa 'Nimemkaribisha Nyoka'. Unaelezea moja ya matatizo yanayoweza kutokea kwenye ndoa. Ni kisa cha kusikitisha kinachoeleza juu ya mwanamume aliyekuwa na mpenzi wake nje ya ndoa. Akaona haitoshi, akataka kumpeleka kabisa nyumbani kwake kuwa mkewe. Akapiga plani zake akishirikiana na mpenzi wake wakaamua kuitana mtu na dada yake. Mwanamke akajifanya ametoka kijijini akaja kwa mpenzi wake, akapokewa na mama mwenye nyumba. Wakaishi kwa muda mrefu kama mtu na wifi yake. Ukweli haikuwa hivyo bali walikuwa mtu na mke mwenzake. Siku mke alipokuja kujua 'kulichimbika'.

**Hebu tutembee na mashairi ya wimbo huo;-**

*"Nimepatwa na mgeni nyumbani kwangu, mume wangu hakuwapo alikuwa kazini, mgeni akajitambulisha ya kwamba yeye ni dada wa mume wangu, na kwamba anatokea nyumbani, kwa wazazi wake kijijini. Nikamkaribisha bila shaka yoyote mama, nikampikia chai na chakula nikampa wifi yangu."*

Plani iliyopangwa ni hiyo. Mtu aliyeanza kwenda nyumbani hapo ni yule hawara. Mwanamume yeye alijifanya kama hajui kitu. Na wala hakumwambia mkewe kuwa dada yake atamtembelea. Wimbo ukaendelea. *"Mume wangu alipotoka kazini nikamweleza mambo yote mama hee, naye akakubali kwamba ni dada yake ambaye wamezaliwa tumbo moja lele, basi tukaendelea kuishi kama vile mtu na wifi yake ndani ya nyumba, bila matatizo yoyote mama hee."*

Jamaa alivyorudi kutoka kazini alijifanya hajui chochote, akamkuta tu mgeni, wimbo haukueleza, lakini ikaonekana alipofika na kumkuta akasema "Waoo dada umekuja, habari za kijijini." Hii ni kuongeza uzito mke akubali kama ni dada yake. Wimbo unaendelea.

*"Aaaaa, kumbe nilikuwa nakula na nyoka sikujua, aaaa, kumbe nilikuwa nakula na nyoka sikujua."*

Jinsi wimbo huu unavyoimbwa, inaonekana ni kwamba tukio limeshafanyika, ndiyo anasimulia mkasa uliompata, ndiyo maana anasema kumbe alikuwa anakula na nyoka ila hakujua.

Mwishoni anajuta kwa kusema kumbe alikuwa amemkaribisha nyoka

*"Nimemkaribisha nyoka eee, kumbe nimemkaribisha nyoka eee, Salima nilidhania wifi yangu, kumbe ni mke mwenzangu mama."*

Hapa mwishoni tunapata jina la mwanamke huyo fedhuli aliyekwenda nyumbani kwa mwenzake na kuitikisa ndoa ya mwenzake, anaitwa Salima. Hii na mingine ni mikasa inayojitokeza sana kwenye jamii, ambayo wanamuziki wa zamani wamekuwa wakisimulia kwa njia ya kuhabarisha, kuburudisha na kuelimisha pia.

Haya mambo si lazima yatokee kwenye ndoa na wengine hayatowatokea kabisa, lakini kwa uchache visa kama hivi vipo na ni moja ya changamoto nyingi kwenye ndoa zinazowapata wote wawili, mke na mume. Visa vipo vingi sana, leo nimeweka hiki kimoja, nitaendelea kuwaletea visa vingi kwenye ndoa vilivyoimbwa na wanamuziki wa dansi nchini Tanzania.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na walipomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-10

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

ALIIPAKI gari yake maeneo ya wazi Mwanyamala Mwinjuma. Akaanza kutembea kwa miguu, kukatiza Kanisa la Pentekoste, Manjawila, hadi Maduka Matatu. Hakuwa mwenyeji sana huko, ila aliifuata barabara iliyokuwa ikielekea Kwa Kidile na kushuka Bonde, kabla ya kupandisha maeneo ya Magomeni Makanya.

Aliambiwa akifika Maduka Matatu mbele kuna Jengo la Serikali za Mitaa. Na kweli baada ya kutembea kwa muda kidogo alikutana na maandishi hayo. Na hapo hapo kulikuwa na kona, iliyoacha barabara kubwa, na kuingia njia ndogo, lakini iliyoweza kupitisha hata gari ndogo.

Nyumba ya kwanza tu kushoto alikutana na maandishi mengine, ikionyesha ni jengo la zahanati. Akakumbuka aliambiwa nyumba ya Hidaya inapakana na zahanati hiyo upande wa kulia kwake.

Ilikuwa ni saa 2:30 usiku. Prince aliwahi zaidi kuliko muda alioambiwa kuutumia kuifanya kazi hiyo.

Muda atakaoutumia kwanza ni kusoma mazingira na kuangalia aingie vipi? Alijipitisha na kwenda mbele, halafu akarudi na kukaa kwenye benchi nje, akijifanya ni mmoja wa watu wanaosubiri huduma ya kutibiwa.

Baada ya kuhakikisha watu wote wanaohitaji kutibiwa wameisha na kubaki yeye, aliinuka kwenye benchi na kuifuata nyumba ile aliyoambiwa.

Alipofika kwenye mlango wa bati, alipousukuma ulipiga kelele, lakini haukufunguka. Ulikuwa umefungwa. Kelele za bati zilisikika ndani. Halafu ikasikika sauti "Ngoja Hasnat aje kukufungulia." Ilisikika sauti ya kike iliyoonyesha ni mama mtu mzima kidogo.

Ilisikika miguu iliyochangamka kwa kutembea kwa haraka ikija kufungua. Bila tahadhari wala kuangalia, alionekana kurudi tena ndani bila kuangalia ni nani anaingia.

Tayari alishapata picha kuwa huenda kuna mtu mmoja yoyote yule ambaye huwa anakuja mida hiyo, lakini bado hajafika. Hivyo ilibidi aingie kwa tahadhari. Baada ya kuingia kwenye mlango mkuu wa bati, sasa aliuelekea mlango wa kuingilia ndani.




**Tayari alishapata picha kuwa huenda kuna mtu mmoja yoyote yule ambaye huwa anakuja mida hiyo, lakini bado hajafika. Hivyo ilibidi aingie kwa tahadhari. Baada ya kuingia kwenye mlango mkuu wa bati, sasa aliuelekea mlango wa kuingilia ndani.**

Alichomoa bastola yake tayari kwa kuitumia. "Mlango mbona uko wazi." Ilisikika sauti ile ile ya mwanzo iliyomtuma mtu kufungua. Nadhani ni baada ya kuona mtu aliyefunguliwa anachelewa kuingia.

Ramani ya ndani tayari alishaambiwa na baba yake kuwa ni nyumba ya vyumba viwili na sebule.

Na kwa jinsi ilivyo ni kwamba unapoingia ni sebuleni na upande wa kulia na kushoto ndiyo kuna vyumba.

Kwa kasi ya umeme aliingia ndani kiasi cha kuwashtua waliokuwa humo.

"Mikono juu na nyamaza. Atakayepiga kelele nammaliza hapa hapa." Akaunguruma.

Japo kulikuwa na mwanga hafifu wa taa ya umeme ya balbu, lakini Prince aliona vema.

Kulikuwa na wanawake wawili tu humo ndani. Wote walikuwa sebuleni. Mmoja ni mtu mzima na mmoja ni msichana anayeonekana kuwa na umri usiozidi umri wa miaka 22.

Walinyanyua mikono juu, huku sura zao zikitawaliwa na mshangao uliochanganyikana na hofu.

"Hakuna mtu yoyote humo vyumbani?" Akauliza.

"Hakuna baba." Akajibu mama kwa woga.

"Wewe ndiye Hidaya?" Akauliza tena. "Ndiyo mimi." Akajibu kwa kigugumizi.

Ilimchukua dakika nzima Prince akiwatazama. Baba yake alimtuma amuue Hidaya. Lakini amemkuta na mtu mwingine. Akimuacha anaweza kuwa msaada mkubwa kwa polisi kuwezesha yeye kutiwa mbaroni.

Akajiuliza aue wote wawili au mmoja? Akiua wawili ni kwamba atakuwa ameua mtu mwingine asiye na hatia.

"Huyu ni binti yako?"

"Ndiyo huyu binti yangu, anaitwa Hasnat, ni huyu huyu tu mmoja ninaye." Alijibu kwa woga.

"Ila usituue." Aliongea kwa kuomboleza.

Macho na akili ya Prince haikuwa kwa mama yule anayelalamika. Yule aliyeambiwa amuue.

Yalikuwa kwa binti yake. Alimuangalia kwa dakika mbili. Alimuangalia tena kwa makini, licha ya mwanga hafifu. Alikuwa anamtazama msichana huyo aliyekuwa anatoa macho na kufumba kwa hofu ya kuuawa, akiwa ameinua mikono juu. Zilipita dakika tano bado Prince alikuwa hajafyatua risasi. Hii ni kwa mara ya kwanza tangu apewe kazi hiyo na baba yake. Kazi ya kulipa kisasi cha kudhulumiwa shamba mama yake na baadaye kuawa na watu hao. Wakaiba pia nyaraka. Mwenyewe alionekana kuifanya kwa ari na bidii kubwa. Akaona fahari kumlipia kisasi mama yake ambaye hakuwahi kumuona. Ameonyeshwa kwenye picha tu.

Kwa mara ya kwanza alihisi kitu ambacho hakuwahi kukihisi kwenye maisha yake yote.

"Huruma? Akajiuliza "Hapana." Akajijibu mwenyewe. Hakuwahi kuwa na huruma kwenye suala hili. "Sasa ni nini?" Hakuwa na jibu lolote.


Sabri na Hussein aliwamaliza kwa sekunde chache tu kwa risasi. Nassor na Hassan aliwamaliza kwa kutengeneza ajali iliyotokana na risasi zake mbili kupiga magurudumu ya nyuma ya gari walilokuwa wamepanda. Leo huyu mwanamama, akiwa na binti yake mbona imekuwa ngumu?

Hisia zilizomuingia kichwani mwake zilisababisha mikono yake kufa ganzi, na ikaanza kukosa nguvu. Taratibu akaishusha bastola yake. Akaiweka mfukoni.

Licha ya kwamba hakuna binadamu anayetaka kufa. Jinsi alivyoingia mtu yule mle ndani na kuonyesha sura yenye dalili zote za kuua na ukatili, lakini kitendo cha kurudisha bastola mfukoni kiliwashangaza Hidaya na binti yake Hasnat. Hawakujua aliyetaka kuwatwanga risasi amepatwa na matatizo gani. Waliendelea kuomba Mungu aendelee hivyo hivyo, asiwabadilikie.

Lakini bado walikuwa na hofu, kwani hawakujua hali ile ya kuonekana kughairi ingemchukua muda gani.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# YAMETIMIA

## Sasa mke na mume

HATIMAYE wanamuziki nyota wa Bongo Fleva, Billnas na Nandy sasa ni mke na mume baada ya kufunga ndoa katika kanisa la KKKT jijini Dar es Salaam jana.

Harusi hiyo ambayo ilikuwa ikionyeshwa moja kwa moja na baadhi ya vituo vya televisheni na mitandao ya kijamii, imekuwa gumzo kutokana na umaarufu wa maharusi hao.

Wakiwa mbele ya mchungaji wa kanisa, wanandoa hao kila mmoja aliapa kumtunza mwenzake kwa shida na raha na kisha kuvishana pete kama alama ya upendo na uaminifu.

Kwa wiki kadhaa Nandy na Billnas wamekuwa katika mijadala mikali na wafuasi wa burudani baada ya kutangaza wapo mbioni kufunga ndoa, hata hivyo hawakutaja siku ambayo wangekula kiapo hicho.

Wengi waliokuwa wakiangalia moja kwa moja sherehe hizo za harusi, waliwapongeza wawili hao kuingia katika maisha mapya kama mke na mume na kuwataka kuwa wavumilivu katika maisha yao.

# Dick Flavour atambulisha 'Nitakutumia' kibabe

MWANAMUZIKI anayekuja kwa kasi katika muziki wa Bongo Fleva, Dick Flavour, ametambulisha kibao kipya kinachoitwa 'Nitakutumia'katika miondoko ya singeli.

Akizungumza na Nipashe jana, Dick Flavour, amesema wimbo huo ambao amemshirikisha Tizo Dash umetengenezwa na Prodyuza Adasco chini ya studio ya J4d sound.

"Mashabiki zangu natumaini mtaupokea kwa furaha wimbo wangu 'Nitakutumia' kwani una ladha tofauti. Nawashukuru kwa kuniunga mkono katika kipaji changu naomba muendelee kuwa mashabiki imara," amesema Dick Flavour.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**KOUNDE ANUKIA CHELSEA**

KLABU ya Chelsea imefufua nia yao ya kumnunua mlinzi wa Sevilla, Jules Kounde, 23, baada ya Manchester City kuamua kutomuuza mlinzi wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Nathan Ake (27) kwa timu ya Thomas Tuchel. ***(Guardian)***

**GNABRY ANOGEWA BAYERN**

MATUMAINI ya Chelsea kumsajili Serge Gnabry, 27, wa Bayern Munich yamepata pigo baada ya mshambuliaji huyo wa Ujerumani kuamua kusalia katika klabu hiyo. ***(Football London)***

**LEWANDOWSKI AKARIBIA**

BAADA ya kumpata winga wa Leeds United na Brazil, Raphinha, Barcelona wanapiga hatua katika majaribio yao ya kumsajili mshambuliaji mahiri wa Poland, Robert Lewandowski, 33. ***(The Athletic)***

**PEPE RASMI KUUZWA**

ARSENAL iko tayari kumuuza, Nicolas Pepe, 27, kwa chini ya ada ya rekodi ya klabu ya pauni milioni 72 waliyomlipa, huku winga huyo wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast akiwa sio sehemu ya mipango ya kocha, Mikel Arteta. ***(Diario de Sevilla)***

**LINGARD KUTUA ARABUNI**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United, Jesse Lingard, 29, anafikiria kuhamia Saudi Arabia ambako anaweza kulipwa pauni milioni 10 kwa mwaka. Mkataba wa mchezaji huyo wa England na United ulimalizika mwezi uliopita. ***(Daily Star)***

**ZINCHENKO KITAELEWEKA**

ARSENAL wana matumaini ya kufikia makubaliano ya kumsajili mchezaji mahiri wa Manchester City, Oleksandr Zinchenko, 25. ***(ESPN)***

**CORNET SOKONI EPL**

KLABU ya Everton ipo kwenye mazungumzo na Burnley iliyoshuka daraja ili kumsajili winga wa Ivory Coast, Maxwel Cornet, 25, ambaye alifunga mara tisa katika mechi 26 za Ligi Kuu England. ***(The Athletic)***

**IBRAHIMOVIC MAMBO SAFI**

KLABU ya AC Milan inakaribia kutangaza mkataba mpya kwa mshambuliaji wa Sweden, Zlatan Ibrahimovic mwenye umri wa miaka 40. ***(Football Italia)***


**NEWCASTLE YAMFUATA BROJO**

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Albania, Armando Brojo, 20, bado analengwa na Newcastle United, lakini kocha, Eddie Howe ameonya kuhusu ugumu wa "bei ya juu na upatikanaji mdogo" wa nyota huko kufikia malengo ya kuimarisha kikosi chake. ***(Mirror)***

**SPENCE ASAJILIWA SPURS**

TOTTENHAM Hotspur inakaribia kumtangaza beki wa Timu ya Taifa ya England chini ya umri wa miaka 21, Djed Spence kama usajili wao mkuu wa sita msimu huu wa joto. Mchezaji huyo wa Middlesbrough amefanyiwa vipimo vya afya katika klabu hiyo ya Ligi Kuu England kabla ya kununuliwa kwa pauni milioni 15. ***(Sky Sports)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# KOULIBALY RASMI MALI YA CHELSEA

**LONDON,** England

### Beki huyo afurahia kutua Stamford Bridge na kusema...

CHELSEA imekamilisha usajili wa Kalidou Koulibaly kutoka Napoli kwa dau la euro milioni 40, huku beki huyo wa kati wa Timu ya Taifa ya Senegal akisaini mkataba wa miaka minne hapo Stamford Bridge.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 anakuwa mchezaji wa kwanza kati ya safu ya ulinzi inayotarajiwa na Chelsea baada ya kuondoka kwa Antonio Rudiger na Andreas Christensen waliomaliza mikataba yao.**

Ingawa mara zote amekuwa chaguo, klabu hiyo ya London ilimgeukia kinara huyo wa Napoli baada ya mlengwa wa kipaumbele, Matthijs de Ligt kutoweza kufikia.

Kinachoshangaza ni Juventus walitaka Koulibaly achukue nafasi ya De Ligt anayekwenda Bayern Munich, lakini ikashindikana.

Hilo liliwapa Chelsea faida, na The Blues wameharakisha kukamilisha dili la euro milioni 40 kwa ajili ya beki huyo, ambaye ametia saini mkataba utakaodumu hadi 2026.

Baada ya kufaulu vipimo vya afya kule London, Koulibaly alisafirishwa hadi Las Vegas kuungana na wachezaji wenzake wapya kwenye ziara yao ya kujiandaa na msimu mpya na jana alitambulishwa rasmi kama mchezaji wa Chelsea.

"Nina furaha sana kuwa hapa na timu hii Chelsea," alisema Koulibaly akiiambia tovuti ya Chelsea.

"Ni timu kubwa duniani na ndoto yangu ilikuwa ni kucheza Ligi Kuu England, Chelsea walikuja kwanza mwaka 2016 lakini hatukufanikiwa, sasa walipokuja kwangu nilikubali kwa sababu walinihitaji sana.

"Nilipozungumza na marafiki zangu wazuri Edou (Edouard Mendy) na Jorginho walifanya uchaguzi wangu kuwa rahisi kwa hivyo nina furaha sana kuwa hapa.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 288.
MECHI KALI
BRUGGE
VERSUS
KAA GENT
1 | 2.09
X | 3.43
2 | 3.04
PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# MAHREZ AAMUA KUZEEKEA MAN CITY

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester City, Riyad Mahrez amesaini mkataba wa kubakia kwenye viunga vya klabu hiyo hadi mwaka 2025.

Mahrez alisajiliwa na Manchester City mwaka 2018 akitokea Leicester City katika uhamisho uliogharimu kiasi cha pauni milioni 60, tangu asajiliwe amefanikiwa kucheza mechi 189, na kufanikiwa kufunga mabao 63, na kusaidia kupatikana magoli 43 kwenye mashindano yote.

"Nina furaha kubwa kusaini mkataba mpya. Nimekuwa nikifurahia kila dakika kwenye muda wangu hapa. Ni fahari kuwa sehemu ya klabu bora isiyoelezeka," alisema Mahrez.

Katika miaka yake minne aliyotumia hapo City, amefanikiwa kushinda mataji manne ya Ligi Kuu England, makombe matatu ya Ligi na ubingwa mara moja wa Kombe la FA.



## Raphinha amtaja Ronaldinho amechangia kusajiliwa Barca

**BARCELONA,** Hispania

RAPHINA amekiri kumtazama nyota Ronaldinho akiwa na Barcelona katika miaka ya 2000 kulimfanya kutaka kuiga ubora wake na kutaka kuichezea klabu hiyo.

Winga huyo alikamilisha uhamisho wake wa kwenda Camp Nou juzi baada ya kukataa ofa ya Chelsea akitoka Leeds United.

Akizungumza kwenye sherehe yake ya utambulisho, Raphinha alifichua mapenzi yake kwa Ronaldinho yalikuwa na ushawishi juu ya alikotaka kwenda baada ya kuondoka Elland Road.

"Nilianza kuitazama Barca wakati Ronaldinho alipokuja hapa. Kila kitu alichofanikisha hapa hakika kiliongeza hamu ya kuja hapa. Siku zote nilitaka kuja hapa," alisema Raphinha .

"Siku zote nilikuwa na matumaini siku moja nitaweza kutimiza ndoto yangu tangu nilipokuwa mtoto, kuunda sehemu ya timu kama Barca.

"Sote tuna njia zetu tofauti za uchezaji bila shaka kwa hiyo mimi ni tofauti sana na Ronaldinho."

,541,640

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 20/7/22 | 18:00 | CA Fenix vs Mvo Wanderers | 2.39 | 3.02 | 3.12 |
| 2. 20/7/22 | 20:00 | Maccabi Haifa vs Olympiakos | 3.16 | 3.11 | 2.37 |
| 3. 20/7/22 | 20:00 | San Lorenzo vs Union Santa Fe | 2.44 | 3.18 | 3.07 |
| 4. 20/7/22 | 20:00 | Botev Plovdiv vs Apoel Nicosia | 2.88 | 3.23 | 2.42 |
| 5. 20/7/22 | 21:00 | Dynamo Kiev vs Fenerbahce | 2.75 | 3.30 | 2.55 |
| 6. 20/7/22 | 21:15 | Maribor vs Sheriff Tiraspol | 2.79 | 3.09 | 2.64 |
| 7. 21/7/22 | 01:00 | Goias vs Fluminense | 3.24 | 3.19 | 2.26 |
| 8. 21/7/22 | 01:00 | CSA AL vs Cruzeiro | 3.18 | 2.93 | 2.41 |
| 9. 21/7/22 | 01:00 | Defensa Justicia vs Independiente | 2.30 | 3.23 | 3.28 |
| 10. 21/7/22 | 02:30 | Internacional vs Sao Paulo | 2.34 | 3.14 | 3.14 |
| 11. 21/7/22 | 03:30 | Lanus vs Velez Sarsfield | 2.82 | 3.12 | 2.67 |
| 12. 21/7/22 | 05:05 | Guadalajara Chivas vs Club Leon | 2.26 | 3.24 | 3.19 |
| 13. 21/7/22 | 20:30 | Aris Limassol vs Neftchi Baku | 2.37 | 3.16 | 3.01 |


MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI- 17/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3030 | Vasteras SK vs Landskrona Bois | 2.11 | 3.52 | 3.31 |
| 15:00 | 1051 | Torpedo Moscow vs Sochi | 3.55 | 3.40 | 1.98 |
| 15:00 | 4391 | Lyngby vs Silkeborg | 3.71 | 3.66 | 1.88 |
| 15:00 | 5811 | Viborg FF vs Aalborg | 2.27 | 3.51 | 2.86 |
| 16:00 | 2337 | Hammarby vs Elfsborg | 1.92 | 3.64 | 3.29 |
| 16:00 | 2566 | Wisla Plock vs Lechia Gdansk | 2.60 | 3.24 | 2.46 |
| 16:00 | 2607 | Halmstads BK vs Utsiktens BK | 1.65 | 3.98 | 4.90 |
| 16:00 | 2947 | Seinajoen JK vs Ilves Tampere | 2.24 | 3.14 | 2.99 |
| 16:00 | 3736 | IFK Goteborg vs Mjallby | 1.96 | 3.28 | 3.52 |
| 16:00 | 3770 | Sirius FK vs Degerfors | 1.81 | 3.72 | 3.58 |
| 16:00 | 4150 | AIK Football vs Kalmar | 1.74 | 3.33 | 4.41 |
| 16:00 | 4674 | Tampere United vs FC Jazz | 2.10 | 4.04 | 2.66 |
| 16:00 | 4809 | Spartaks Jurmala vs FK Liepaja | 6.67 | 4.61 | 1.36 |
| 17:00 | 1808 | Slutsk vs Dinamo Brest | 2.11 | 3.03 | 3.37 |
| 17:00 | 2987 | SpVgg Purgstall vs Admira Wacker | 17.69 | 10.81 | 1.05 |
| 17:00 | 3137 | Bonnyrigg Rose vs Hibernian | 15.76 | 7.68 | 1.10 |
| 17:00 | 4351 | Juventude RS vs Goias | 1.99 | 3.14 | 3.58 |
| 17:00 | 4602 | Copenhagen vs Horsens | 1.31 | 5.02 | 9.04 |
| 17:15 | 1021 | Paide Linnameeskond vs Parnu JK Vaprus | 1.11 | 7.43 | 14.66 |
| 17:30 | 3461 | Lokomotiv Moscow vs Nizhny Novgorod | 1.73 | 3.56 | 4.51 |
| 17:30 | 4029 | FC Lugano vs FC Sion | 1.91 | 3.46 | 3.82 |
| 17:30 | 4587 | Servette Geneva vs St. Gallen | 2.33 | 3.68 | 2.67 |
| 17:55 | 4539 | Dziugas vs Banga Gargzdai | 2.46 | 3.30 | 2.70 |
| 18:00 | 2349 | PKS Olimpia Elblag vs KS Gornik Polkowice | 2.67 | 3.16 | 2.45 |
| 18:30 | 4621 | FK Radnicki 1923 vs Mladost Lucani | 2.65 | 3.30 | 2.50 |
| 18:30 | 5508 | Pogon Szczecin vs Widzew Lodz | 1.49 | 3.93 | 5.70 |
| 19:00 | 1064 | Brondby vs Aarhus | 1.97 | 3.40 | 3.65 |
| 19:00 | 1194 | Odd Ballklubb vs Lillestrom | 2.86 | 3.37 | 2.33 |
| 19:00 | 1462 | Switzerland W vs Netherlands W | 6.87 | 4.62 | 1.36 |
| 19:00 | 1583 | Sarpsborg vs Valerenga | 2.08 | 3.57 | 3.17 |
| 19:00 | 2569 | Molde vs Haugesund | 1.43 | 4.74 | 6.05 |
| 19:00 | 2655 | Viking vs Kristiansund | 1.29 | 5.62 | 8.03 |
| 19:00 | 2844 | Sweden W vs Portugal W | 1.34 | 4.72 | 7.09 |
| 19:00 | 2890 | Dunajska Streda vs Liptovsky Mikulas | 1.47 | 4.21 | 5.49 |
| 19:00 | 4049 | Brugge vs KAA Gent | 2.09 | 3.43 | 3.04 |
| 19:00 | 4394 | Vestmannaeyjar vs Valur | 3.63 | 3.53 | 1.85 |
| 19:00 | 4840 | Tromso vs Stromsgodset | 1.78 | 3.71 | 4.12 |
| 19:00 | 5053 | MFK Skalica vs Ruzomberok | 3.88 | 3.43 | 1.82 |
| 19:30 | 1813 | El Gouna vs Talaea El Gaish | 3.28 | 2.72 | 2.48 |
| 19:30 | 2978 | Flora Tallinn vs Tallinna Kalev | 1.01 | 12.78 | 29.48 |
| 19:30 | 4479 | Smouha Club vs National Bank | 2.12 | 3.27 | 3.37 |
| 19:30 | 5670 | La Serena vs Antofagasta | 2.19 | 3.19 | 3.04 |
| 20:00 | 1028 | FC Krasnodar vs Fakel | 1.66 | 3.76 | 4.71 |
| 20:00 | 3444 | Finn Harps vs Derry City | 4.51 | 3.63 | 1.66 |
| 20:00 | 4568 | Dinamo Moscow vs Rostov | 1.79 | 3.54 | 4.19 |
| 20:00 | 4932 | Sligo Rovers vs UCD Dublin | 1.35 | 4.50 | 7.25 |
| 21:00 | 1334 | Aalesunds vs Rosenborg | 2.86 | 3.31 | 2.37 |
| 21:00 | 3943 | FK Napredak vs FK Vozdovac | 2.34 | 3.24 | 2.75 |
| 22:00 | 1082 | Arab Contractors vs Ceramica Cleopatra | 3.07 | 2.67 | 2.67 |
| 23:40 | 4504 | Almirante Brown vs Club Almagro | 2.18 | 3.00 | 3.24 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# MAGEREZA MORO YAIPA KICHAPO POLISI ARUSHA

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya netiboli ya Magereza Morogoro imepata ushindi wa mabao 51-34 dhidi ya Polisi Arusha katika mechi ya Ligi Daraja la Kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ndani wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana asubuhi.

**Licha ya Magereza kupata ushindi, lakini haikuwa rahisi kutokana na ushindani walioupata kutoka kwa wapinzani wao.**

Kocha Mkuu wa Magereza Morogoro, Winfrida Emmanuel alisema anashukuru Mungu amepata ushindi huo kwa kumfunga mpinzani wake idadi kubwa ya magoli.

Winfrida alisema siri ya mafanikio yake katika mechi hiyo ni kufanya mazoezi ya muda mrefu pamoja na nidhamu nzuri waliyokuwa nao wachezaji wake.

"Tunamshukuru Mkuu wa Jeshi la Magereza Tanzani, Selemani Mzee kwa kuhakikisha tumeweza kushiriki mashindano haya," alisema Winfrida.

Naye Kocha Mkuu wa Polisi Arusha, Emerenciana Silas, alisema kilichowafanya wasipate matokeo mazuri katika mchezo huo ni wachezaji wake kutokuwa na uzoefu wa mashindano hayo.

Alisema mchezo ulikuwa mgumu na kuongeza wapinzani wao walisaidiwa na uzoefu waliokuwa nao.

"Tumeshindwa kupata matokeo mazuri kwa sababu timu yangu ni chanya, haina uzoefu na mashindano makubwa kama haya, ni mara ya kwanza tunashiriki, binafsi sijakata tamaa nina imani nitafanya vizuri katika mchezo ujao," kocha huyo alisema.

Katibu Mkuu wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), Rose Mkisi alisema watatumia mashindano hayo kupata kikosi kizuri ya Timu ya Taifa.

Mkisi alisema mashindano ya msimu huu yamekuwa mazuri na yenye ubora kutokana wadhamini walivyojitoa kuwasaidia.

"Mashindano haya yana msisimko mkubwa, timu zote zinacheza kiushindani lengo letu ni kupata timu bora ya taifa na timu nne ambazo zitashiriki michuano ya Muungano," alisema Mkisi.



Kocha Mkuu wa Simba Mserbia, Zoran Manojkovic (kulia), akimwongoza beki wa kati wa timu hiyo, Erasto Nyoni katika mazoezi yanayoendelea kwenye mji wa Ismailia nchini Misri ambapo Wekundu wa Msimbazi wameweka kambi kujiandaa na msimu mpya. **PICHA: SIMBA SC**

# *Nyota saba kutemwa Ruvu Shooting*

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Ruvu Shooting haitakuwa na wachezaji wake tisa iliowatumia msimu uliomalizika kwa sababu wawili wamepata timu nyingine huku wakifikia uamuzi wa kuachana na nyota saba, imefahamika.

Katibu Mkuu wa Ruvu Shooting, Ramadhani Dikala alisema baada ya kukaa kikao na benchi la ufundi ambalo liko chini ya Kocha Mkuu, Boniface Mkwasa, wameamua kuachana na wachezaji hao na kuanza mipango ya kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

"Wiki iliyopita tulikaa na benchi la ufundi, katika ripoti yake ametaka wachezaji saba waachwe, lakini wapo wawili wameondoka, wamepata timu kwa hiyo idadi imeongezeka kutoka saba hadi tisa," alisema Dikala.

Aliongeza baada ya mchakato huo wa usajili kukamilika watatangaza wachezaji wapya na ambao wameachana nao huku akiweka wazi nyota wake, Nathaniel Chilambo amesajiliwa na Azam FC.

Kuhusu maandalizi ya msimu ujao, baada ya kunusurika kushuka daraja, Katibu huyo alisema kikosi chao kitaingia kambini wakati wowote na wanachosubiri ni kukamilika kwa zoezi la usajili.

Michezo
Jumapili Julai 17, 2022
Nipashe



Koulibaly mali ya Chelsea UKURASA 21



Wachezaji wa Simba ya jijini Dar es Salaam wakifanya mazoezi katika mji wa Ismailia nchini Misri ambapo wameweka kambi kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2022/2023 na michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: SIMBA SC**

# SIMBA YASHUSHA MAJEMBE MAPYA

## Ni kiungo Mnigeria, beki kisiki huku wakitarajia...

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha inarejesha ufalme wake uliopotea katika msimu uliopita na kufanya vizuri kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba inatarajia kumsajili beki mpya kutoka Burkina Faso, Mohammed Ouattara, imefahamika.

**Ujio wa Ouattara ni mapendekezo ya Kocha Mkuu wa Wekundu wa Msimbazi, Zoran Manojkovic kwa ajili ya kuchukua nafasi iliyoachwa na Paschal Wawa, ambaye tayari ameshajiunga na Singida Big Stars inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Nyota mwingine ambaye pia yuko Misri na kikosi hicho na anatarajiwa kutambulishwa rasmi hivi karibuni ni kiungo mshambuliaji Mnigeria Nelson Okwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez alisema mchakato wa usajili kuelekea msimu mpya umekamilika kwa asilimia kubwa na kila kitu kimefanyika kwa kushirikiana na Zoran.

Barbara alisema kocha alitoa baraka ya kusajili baada ya kuwaangalia wachezaji kupitia picha za video mbalimbali walizocheza nyota hao na baadhi ya michezo ambayo Simba ilicheza hivi karibuni na kutoa mapendekezo.

"Hauwezi kusajili tu kiholela, tunasajili kwa mipango na kuziba madhaifu na kile tulichokikosa katika msimu uliopita, Simba lazima tuhangaike kusajili kulingana na mahitaji yetu," alisema Barbara.

Aliongeza uamuzi wa kuipeleka timu Misri kwa ajili ya kuweka kambi Misri kuna faida, kwa sababu timu yao inajiandaa kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na huko (kwa Waarabu), ndipo wapinzani wao wanapotoka.

Alisema mbali na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba imedhamiria kuendelea kufanya vizuri katika michezo ya kimataifa, hivyo ni lazima waweke kambi mahali ambapo watapata michezo ya kirafiki itakayowasaidia kwa ajili ya kukabiliana na ushindani ulioko mbele yao.

"Katika hoteli na kambi iliyofikia Simba, kuna Timu ya Taifa ya vijana ya Misri (U-20)na Pyramids, pia katika mji huo kuna timu ambazo zimekuja kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa ligi ya nchi hiyo, tayari tumeshaanza mazungumzo na hizo timu ikiwamo kwa ajili ya kupata michezo ya kirafiki kulingana na ratiba za kocha Zoran, tunatarajia wiki ijayo tutaweka wazi siku na mechi tulizopata," alisema Barbara.

Aliongeza kuhusu wachezaji ambao Simba itaachana nao hasa nyota wa kigeni, jukumu hilo ameachiwa kocha kwa kuwapa fursa ya mwisho ya kuwaangalia katika kipindi hiki cha 'Pre Season'.

"Lazima tutumie fursa ya Pre Seoson kuangalia hadhi ya wachezaji wetu, mwalimu atatumia muda wa kutosha kuangalia wachezaji, hapo ndio ataamua nani na nani wataendelea na timu au kuondoka, ila kikubwa bado usajili unaendelea," alisema Barbara.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Simba, Ahmed Ally alisema kila kitu kinaenda sawa katika kambi hiyo na wachezaji wote wanafurahia mazingira waliyoko.

Ahmed alisema kikosi chao kilianza rasmi mazoezi kuelekea msimu mpya hapo juzi na wanaamini mechi za kirafiki watakazocheza kuanzia wiki ijayo zitawasaidia kuwaimarisha.

Kikosi hicho cha Simba kitarejea nchini mapema mwezi ujao tayari kushiriki Tamasha la Simba Day na baadaye kuwakabili Yanga katika mchezo wa Ngao ya Jamii utakaochezwa Agosti 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

## Yanga yajitabiria neema Ligi Bara

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

WAKATI wachezaji wake iliowasajili kuelekea msimu mpya wakikutana pamoja kwa ajili ya kuanza kambi, uongozi wa Yanga umetamba wamefanya usajili mzuri kuliko timu nyingine za hapa nchini na kuwataka wapinzani wao wasubiri kupokea vichapo mfululizo.

Yanga imesema hakuna timu yenye wachezaji bora kama ambao wao wamefanikiwa kuwanasa.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Msemaji wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema baadhi ya wachezaji tayari wapo kambini tangu juzi akiwamo nyota mpya, Stephane Aziz Ki.

Bumbuli alisema nchi na sehemu ambayo watakwenda kuweka kambi wataitangaza rasmi hivi karibuni.

Aliongeza wako katika majadiliano ya wapi watakwenda kuweka kambi, lakini kesho (leo), watatangaza wapi wanakwenda kuweka kambi mpaka kkuelekea kilele cha Siku ya Wananchi hapo Agosti 6, mwaka huu.

"Tunaangalia kambi tuweke wapi? Nje ya Bara la Afrika, na kama hivyo ni wapi, na tukienda huko kutakuwa na tija? Na kwa kipindi hiki kifupi tulichonacho tunaweza kwenda kufanya maandalizi huko? Hilo ndilo suala ambalo tumekuwa tukijadiliana twende nje ya Afrika au kambi iwe humu humu Afrika na kama ni humu, tukakae wapi?," alisema kiongozi huyo.

Kuhusu mchakato wa usajili, aliweka wazi tayari Yanga imeshakamilisha zoezi hilo na wamejipanga kuendeleza ushindani kama walivyofanya katika msimu uliopita.

"Msimu uliopita ulikuwa mgumu na wenye ushindani licha ya kuwa tulifanikiwa kupata ubingwa wa Ligi Kuu Bara, Kombe la FA na Ngao ya Jamii ambayo tuliibeba mwanzoni mwa msimu," Bumbuli aliongeza.

Awali Yanga ilitarajiwa kuweka kambi yake Uturuki lakini mipango ghafla ikibadilika wakati tayari Simba imepiga kambi katika mji wa Ismailia, Misri huku Azam FC yenyewe itaelekea katika mji wa El Gouna nchini humo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >